

NGUVU ZA KUGEUZWA



[Ndugu Branham na kusanyiko wanavumisha *Amini Tu—Mh.*]

² Ingekuwa kwa namna fulani ni vigumu kwa mtu yeyote kujieleza wenyewe ka—katika wakati kama huu, kusema jinsi ninavyothamini mno majaliwa haya ya kuwa hapa asubuhi ya leo, na—na kuwa miongoni mwenu, kuhudumu Neno la Mungu, ambalo nina hakika mnalifahamu. Na—na ninataka kumshukuru Ndugu Leo na Ndugu Gene, na ninyi watu wote, kwa ajili ya nafasi hii nzuri sana.

³ Na wakati nilipokuwa nikisikiliza wi—wimbo wa kwanza, hadi wa mwisho, kuna kitu fulani kuhusu kuimba huko, ni ibada ambayo kwa kweli huwezi kabisa kuipata tena. Na daima ni majaliwa makubwa kwangu ninapokuja hapa, kama mara moja kwa mwaka, ama mara mbili, kuja ili tu kujazwa na uzuri huo wa hizo nyimbo.

⁴ Nami nilikuwa nikiwazia asubuhi ya leo, wakati Ndugu Leo alipoutangaza ule wimbo wa *Wanakuja Toka Mashariki na Magharibi*, na kuhusu mke wangu kuuimba huo wakati nilipoondoka ku... nilipomwacha na—na Billy na Rebekah, kuanzisha ufufuo huu mkuu, wa utangulizi wake, hasa, uliposambaa katika mataifa. Na halafu nilikuwa nikifikiria, nilipokuwa nikiangalia upande wa pili wa kundi hili zuri la mabibi, wanaonekana waadilifu. Ninakumbuka Meda wakati huo alikuwa ni mmoja wao, alikuwa ni maskini msichana mdogo mwenye nywele nyeusi. Na sasa yeye yuko kama mimi, tunazeeka na kupata mvi, na wakati wetu unaisha. Na hata hivyo tukiwa na Tumaini hili tukufu, kwamba tutakusanyika tena pamoja ndani Yake, mahali ambapo hakutakuwa na wakati tena, uzee, kitu chochote cha kutuzuia wala kutusumbua.

⁵ Siamini ya kwamba ninajua mahali popote ambapo nimepata kupaona maishani mwangu, hasa sana pakiwa na watu wengi namna hii, ambapo palikuwa na Wakristo wengi sana wazuri wenye upendo huu. Msiache kamwe jambo hilo life miongoni mwenu. Hebu kumbukeni tu.

⁶ Nilikuwa nina ninii kidogo... msemo miongoni mwa watu. Jina la mke wangu lilikuwa ni Hope; mke wangu wa kwanza, mamake Billy. Walikuwa wakininii... Tulikuwa watu watatu wakati huo, hao walikuwa ni Hope, na mimi mwenyewe, na Billy. Walikuwa wakituita, “Tumaini, imani, na upendo.” Na kwa hiyo ilionekana kama tuliokuwa na imani shupavu, katika siku hizo, kuamini ya kwamba Neno hili lilikuwa ni kweli; na, yale Mungu aliyokuwa ameahidi, angeyatenda.

⁷ Na, lakini, unaona, “Lililo kuu kuliko haya ni wema, ni upendo.” Kama vile Ndugu Leo alivyosema asubuhi ya leo. “Upendo! Palipo na lugha, zitakoma. Palipo na unabii, utabatilika. Lakini wakati wema, ambao ni upendo, utadumu daima.” Unaona?

Mpenzi Mwana-Kondoo unayekufa, Neno
Lako la thamani
Kamwe halitapoteza Nguvu Zake,
Mpaka Kanisa zima la Mungu lililokombolewa
Litakapookolewa lisitende dhambi tena.

Tangu wakati huo kwa imani nilipokiona kile
kijito
Kilichobubujishwa na majeraha Yako,
Upendo wa ukombozi umekuwa ndio wimbo
wangu,
Na utakuwa huo mpaka nitakapokufa.

⁸ Nafikiri hakuna kitu kilicho kikuu zaidi kuliko upendo. Na upendo, kama hatuwezi kuuelezea . . . Sasa, tunaweza kusema ya kwamba tuna upendo, tunasema tu jambo hilo. Lakini wakati tunapoweza kweli kuonyesha yale tuliyosema kwamba tunayo, ndipo tunayaonyesha ndani yetu.

⁹ Sasa sisi si watu wakamilifu. Tunafanya makosa yetu. Tunafanya mambo yaliyo makosa. Lakini, unaona, upendo hufunika hayo yote. Tuko tayari, tunapona makosa yetu, kurudi na kuombana msamaha. Naam, hao—hao ni mashujaa. Hao, hao ni wanaume na wanawake halisi walio hodari. Mtu yeyote anaweza kutoka nje aende kwenye uwanja wa vita, ambaye ana ujasiri wa kutosha wa kwenda huko; bali wakati anapoangushwa, halafu anaamka na kujaribu tena, unaona. Kulikuwa na wimbo ambao kijana mmoja mwanamume na kijana mwanamke walikuwa wakiimba kanisani, “Kama nikianguka ama kama nikishindwa,” unaona, “Kama nikianguka ama kama nikiininii . . .” Ninasahau jinsi unavyoenda. “Jalia niamke na kujaribu tena.”

Nisamehe, Bwana, na unijaribu mara nyingine
tena. (Unaona? unaona?)
Kama nikianguka ama kama nikitenda
dhambi, jalia niamke na kujaribu tena.
Nisamehe tu, Bwana, na unijaribu mara
nyingine tena.

¹⁰ Na kukiwa na kama watu wapatao mia moja na ishirini hapa kwa wakati mmoja, hamna budi ku—kuona mambo wakati mwingine, adui ataingia ghafla miongoni mwenu, na apitie kwenye mawazo yenu, na—na kuanzisha jambo *hili, lile*. Hebu tulieni tu wakati anapofanya jambo hilo. Kumbukeni ya nyuma, kumbukeni kuhusu asubuhi ya leo, wazieni juu ya nyakati

ambazo mmekeki pamoja katika Ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu.

¹¹ Baadhi yenu ni mafundi bomba na baadhi ni maseremala na wengine *hivi, vile, na vinginevyo*. Mnashirikiana na ulimwengu kila siku, mnapokuwa huko nje. Lakini mnapoona mambo hayo, na majaribu makuu yakiinuka, kumbukeni tu sehemu hizi ndogo, takatifu ambapo mnaketi pamoja, mkiwa na kitu cha pekee kinachodumu. Kazi zenu zitakoma, moja ya siku hizi. Afya yenu itakoma. Hata maisha yenu, hapa duniani, yatakoma. Lakini basi Hicho hakitakwisha. Na kama Yeye ni kiini cha mambo yote, basi hebu na tudumishe nia zetu kwenye Nguzo ya katikati, ile ambayo imetuvuta kwenye jambo hili.

¹² Jamani, kundi hili la watu wazuri, wanaoonekana waadilifu! Simaanishi hasa sana nguo zenu. Nguo zenu ni safi, bila shaka, na kadhalika, nyuso zenu. Nafikiri mabibi hawa wasichana hapa, hakuna rangi ya midomo hata kidogo kwa mmoja wao; wote wakiwa na nywele ndefu, vijana kwa wazee, wa makamu na kadhalika. Naam. Unaona? Vema, ninyi hamtambui tu ni hazina ya jinsi gani mliyo nayo hapa, unaona, katika ibada hii ndogo ya kanisa dogo.

¹³ Ninataka kuwashukuru Ndugu na Dada Shantz, pia, na kwa majaliwa haya ya kuwa nyumbani mwao. Na haya ndiyo makazi yao sasa, kwamba wameuza nyumba yao, nafikiri, huko Canada, nao wameshuka kuja kukaa pamoja nasi. Hatuna tena mali za ulimwengu. Tunautafuta Mji ujao, Ambao Mwenye Kuujenga na Kuubuni ni Mungu.

¹⁴ Na ninamshukuru Ndugu Leo na Gene, kwa jinsi walivyokuwa waaminifu, kwa ono ambalo walipewa wakati tulipokutana mara ya kwanza. Hapana shaka kabisa amewasimulia mara nyingi. Ni ajabu, sikuliona namna hii kabisa. Nilihua kulikuwa na jambo fulani huko mbele. Wakati maskini kijana huyu aliponijia kama nanii... akiwa na ndoto aliyokuwa nayo ya piramidi, nikiwa nimesimama juu kwenye piramidi hii. Naye alipanda akaja mpaka mahali nilipokuwa, nami nilikuwa nimesimama kwenye kisahani, sahani, ama kitu kama nuru.

Akasema, “Ndugu Branham, ulifikaje huko juu?”

¹⁵ Nami nikasema, “Ndugu Leo, Mungu hana budi kumweka mtu katika nafasi hii hapa juu.” Nikasema, “Sasa kwa kuwa umeona, rudi kwa watu na uwaambie ya kwamba unaamini ni la Mungu.”

¹⁶ Wala sikujua hata kidogo wakati huo wakati nilipokuwa kwenye nafasi fulani. Na—nawapenda hawa vijana, nami nilitaka kuwaweka katika nafasi ambapo ningeweza kuwa pamoja nao. Nao walianza kurekodi kanda. Lakini, unaona, nionavyo mimi, wangali wangukuwa wanaendelea kurekodi kanda, nijuavyo mimi. Lakini ni jambo kubwa zaidi jinsi

gani Mungu amewatendea, kuliko kurekodi kanda, unaona. Karibu kila mtu anaweza kurekodi kanda, ambaye ana akili za kufungulia kinasasauti, ama anayeweza kuuza. Lakini inahitaji uongozi wa Roho Mtakatifu kuliongoza pamoja kundi dogo kama hili, asubuhi ya leo, na kuwaweka watu pamoja katika amani na umoja, na wakiwa bado wameshikilia Ujumbe.

¹⁷ Mungu, nakuomba—nakuomba uwajalie, watu hawa, maisha marefu hapa duniani, furaha na shangwe, na halafu “waingie katika furaha za Bwana” mwishoni mwa safari.

¹⁸ Sasa tuko tayari kwa vita, Baragumu Italia. Nyimbo zimekwisha kuimbwa, sasa kunakuja Neno. Nafikiri, ninaposimama hapa, kwamba mnajua. . . Naam, labda mnajua.

¹⁹ Lakini kusikia matamshi haya ya askari hawa vijana hapa! Na mimi mwenyewe ninazeeka, zaidi ya hayo usikilize kwa makini, na imani yako na matumaini, na yale uliyoweka ndani kuuamini Ujumbe ambao—ambao nimepewa na Mungu. Sasa, kama isingekuwa ni kwa ajili yenu nyote, Ujumbe huu usingefaa kitu. Unaona, ina—inapaswa kuwe na mtu fulani wa kuuamini. Na alimuradi tu unatoka kwa Mungu, kutakuwa na mtu fulani atakayeumini, unaona. Mungu amefanya njia. Yeye, ameweka mpango Wake mkuu namna hiyo, ya kwamba, wakati anapotuma kitu Fulani, kuna kitu fulani pale cha kukutana na kitu Fulani hicho. Kilindi huitikia kilindi. Haina—haina budi kuwa hivyo.

²⁰ Ninapenda lile neno ambalo Ndugu Gene alilotumia katika maombi asubuhi ya leo, “Ndani ya nyua Zake tukufu.” Ninajisikia hivyo ninapovuka daraja lile kule chini ku—kuingia mahali ambapo Mungu anatumizwa na kuheshimiwa. Na daima dumisheni hayo namna hiyo. Haidhuru wakati adui. . .

²¹ Sasa kumbukeni, msisahau jambo hili; Ndugu Leo na Gene, hasa. Sasa, mnadhani Shetani ataliacha hili liendeleo namna hii, bila kipingamizi? Loo, la. Hakika hataliacha. Yeye ataenda kuruka na aingie ndani, moja ya siku hizi, kama tu upepo wa kisulisuli. Lakini wakati ninii—wakati adui anapokuja kama mafuriko, Roho wa Mungu huihua beramu dhidi yake. Dumuni tu kujiinua katika maombi mbele za Mungu. Shikamaneni ninyi kwa ninyi. Mshikilieni Mungu. Kwa kuwa, mkipendana, inaonyesha mnampenda Mungu. “Hivi watu wote watajua, ya kwamba ninyi ni wanafunzi Wangu, mkipendana.”

²² Nami nikawazia, muda mfupi uliopita, “Ni uimbaji mzuri jinsi gani! Ni sauti zilizo nzuri jinsi gani! Ni kundi zuri jinsi gani la wanaume na wanawake, waume kwa wake; vijana, wazee, na watu wa makamu, wanaoketi pamoja hapa.” Nikawaza, “Vema, wanapaswa kupata jambo hilo kule Prescott, wanapaswa kwenda kule chini na wanapaswa kufanya matangazo machache ya redio namna hiyo.” Lakini, unaona, hilo lisingekuwa ni lile hasa Mungu alilowaitia vijana hawa kufanya. Unaona? Unaona? Bibi-arusi anaitwa atoke, unaona, anaitwa atoke, sasa kazi

yangu iko huku nje, kuita. Na halafu mambo kama haya, na pale mnapojitenga, na mtu kujishikilia, pale ambapo mnataka kuwalea watoto wenu, kila mmoja akikesha kila siku, kama jicho la tai linavyoangalia makinda yake, ili kwamba msininii... Ukiona jambo lolote baya, basi unamwita mtu huyo kando na kuomba kwa ajili ya jambo hilo, na mambo kama hayo. Lidumisheni safi, takatifu, ili kwamba Roho Mtakatifu aweze kuwa na mahali pa kuzuru.

²³ Mungu anapenda kuabudiwa. Na wakati mnapomwabudu, si hasa kuimba wimbo kama tunavyofanya, bali ni kuuimba katika roho ya ibada, unaona, ndipo unamhisi Roho Mtakatifu akirudi na nguvu mpya.

²⁴ Pia ninamwona kijana mwanamume mkubwa mno hapa, ninawazia tu juu ya ile siku lile kundi la vijana wadogo wakiwa wameketi pale, vijana wanaume na wake zao vijana wameketi pamoja hapa, na mtu mkubwa, mkatili ameketi pale na wanalia tu kama watoto wachanga.

²⁵ Mbona, angalia siku hizi, wako huku nje mtaani, wakiishi katika uzinzi na uchafu wa ulimwengu, na kadhalika.

²⁶ Na kuwazia ya kwamba mnaweza kujitenga na kukusanyika namna hii, ambapo kama yule Mtunga Zaburi alivyosema, "Tazama jinsi ilivyo vema, na kupendeza Ndugu wakae pamoja, kwa umoja." Ni kama mafuta ya kutia yaliyokuwa kwenye ndevu za Haruni, yaliyoshuka mpaka upindo wa mavazi yake. Ambayo, mafuta hayo ya kutia... Ambayo, unajua vile mafuta ya kutia yalivyofanya, yalimfunika kwa ajili ya kuingia katika Uwepo wa Mungu. Unaona, ilibidi atiwe mafuta hayo kabla hajaenda kuingia katika Uwepo wa Mungu. Na wakati ndugu wanapoweza kukaa pamoja katika umoja, inafananishwa na mafuta hayo. Ndipo tunaingia katika Uwepo wa Bwana, tukiwa na upako huo wa ndugu walio pamoja katika umoja. *Mafuta* yanamwakilisha "Roho Mtakatifu."

²⁷ Sasa hebu na tuombe kidogo kabla hatujaingia katika kulisoma Neno.

²⁸ Baba wa Mbinguni, kama vile ndugu yetu alivyoelezea asubuhi ya leo, kuingia katika zile nyua tukufu za Bwana! Sasa, Baba, tunatambua ya kwamba kundi hili la watu hapa, na sasa yale nisemayo, itanibidi kuwajibika kwayo kwenye ile Siku ya Hukumu. Na hili ni watoto Wako. Wabariki, Baba, daima. Wabariki Ndugu Leo na Ndugu Gene. Jalia waongozwe na Roho Wako Mtakatifu, kuwaongoza watu hawa, tunapofanya safari hii kwenda hadi machweo ya jua. Na ndipo, Ee Roho Mtakatifu wa Mungu, tuongoze kwa Mwana. Tujalie, Bwana.

²⁹ Tuvunjie Mkate wa Uzima, kupitia kwenye Neno. Nasi tunaninii... Sasa tunatambua ya kwamba tuko vitani sasa. Tunajivika silaha mbalimbali, hapa nje katika askari hawa, ambazo itawabidi kuzitumia kupigania, katika saa zilizosalia

katika maisha. Nami ninaomba, Bwana, ya kwamba utaweka barabara kila silaha mahali pake, mahali ambapo wanaweza kukingwa dhidi ya a—adui kila mara anapokuja dhidi yao. Tujalie, Bwana. Tunaomba katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

³⁰ Sasa, kwa namna fulani mimi ni mzito katika—katika kuzungumza, kwa sababu mimi si—si mhudumu wa kusomea. Ninajua wako watu hapa walio hodari, wenye akili, wasomi, nao wameweka hayo kando, wapate kuja huku sasa na kupondekapondeka, katika unyenyekevu. Paulo maarufu, yule mtume, ninawazia juu ya maneno yake aliposema ya kwamba, “Sikuja kweni kwa maneno ya kuvutia ya mwanadamu, kwa sababu hapo mngeweka imani yenu kwenye jambo hilo, bali nilikuja kweni katika nguvu za Roho.” Unaona, mambo yale makubwa ambayo alijua alikuwa nayo, aliyaweka kando. Nami ninajisikia asubuhi ya leo, kama huyu mwanamume hapa, kama Ndugu Hughy and dada, mwalimu aliyepo hapa kutoka katika huduma ya utume, na wengi wenu ninyi watu ambao kweli wana akili na ni hodari; na—na mimi ninajisikia duni sana kusimama hapa bila ya elimu zaidi ya niliyo nayo, mbele zenu. Lakini mimi... Na halafu kuona ya kwamba ninyi watu, wa namna hiyo, mnge—mngejinyenyekeza kwa mambo hayo, kuyaweka hayo kando, na kuketi chini na kumsikiliza mtu ambaye ni shida kujua ABC zao, hilo linawafanya kuwa watu wakuu. Si yeye anayeweza kuchomoza nje mabega yake, na kutoka atembea na... Ni yeye anayeweza kujinyenyekeza.

³¹ Nafikiri, tabia, inapimwa kwa...mwanamume, si kwa misuli ya mkono wake wala kwa sugu katika mikono yake, bali kwa kutuna kwa goti la suruali yake ambapo ameomba. Nafikiri hilo ndilo linalomfanya mtu kuwa mwanamume.

³² Sasa nataka kusoma Biblia kidogo, asubuhi ya leo. Na mimi ninapenda Neno. Ninyi je? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Sasa tumemwabudu Bwana, na tutaendelea kumwabudu. Sasa hebu na tumwabudu kama Upanga u—ukatao wenye makali, unapopitia ndani yetu, kuona mahali tunaposimama.

³³ Nami—nami naenda polepole, maana hapa ndipo mahali ninapojisikia ya kwamba ninge—ningeweza kufundisha mambo ninayotaka kusema asubuhi ya leo. Na halafu, bila shaka, Ndugu Leo na Gene, na hao wengine, wata—watayafanyia kazi hayo, tutakapoondoka, na watafafanua mambo muhimu kama nilivyomsikia akitaja kwa moyo wa kupenda sana katika ujumbe wake asubuhi ya leo. Ya kwamba, yeye analipata hilo. Bali huwezi kulisema jambo hilo kutoka kwenye mimbara kama hii ama kwenye kanda, lakini, unaona, hebu keti tu na kuyasoma kwa makini. Endelea tu uyasome, kuyarudia-rudia. Ni vigumu kuyafahamu. Watu wengi sana wanayapata vibaya! Na je! mlijua, enyi kundi do—dogo, ndivyo—ndivyo ilivyo miongoni mwa wanadamu wote? Imekuwa hivyo daima.

³⁴ Kama hawakuweza kumwelewa Bwana na Mwokozi wetu, Yesu Kristo, (hata mitume Wake, unaona) basi tungewezaje kutarajia kulielewa katika siku hii, unaona. Yeye alisema, Yeye angesema mambo ambayo ni magumu, wajua, wala asingeyaelezea. Angeyasema tu. Kasema, kama vile kwa mfano, “Msipoula mwili wa Mwana wa Adamu na kuinywa Damu Yake, hamna Uhai ndani yenu.”

³⁵ Sasa vipi, sasa vipi kama ninii—vipi kama daktari fulani alikuwa amesimama karibu, ama nesi fulani ama yeyote yule, katika kusanyiko hilo, siku hiyo, aliyokuwa akiwazungumzia? Vema, walisema, “Mtu huyu ni mnyonya damu, mnaona, anataka tuinywe Damu Yake.” Unaona, Yeye kamwe hakulielezea. Alilisema tu. Lakini baadaye, Paulo alikuja na kulielezea, jinsi ambavyo ilikuwa ni kufanya ushirika, mwajua, “kuula mwili Wake na kuinywa Damu Yake.” Na kwa hiyo aliyasema tu mambo hayo.

³⁶ Na hatimaye, mwishowe, wale mitume siku moja, hata baada ya kufufuka, kulikuwa na mmoja aliyeegemea begani Mwake, Yohana aliyempenda. Alikuwa kijana mwanamume. Naye alisema, “Imewapasaje kama mtu huyu akikaa mpaka nijapo?” Likaenea neno miongoni mwao, ya kwamba Yohana hata—hatakufa mpaka Yesu atakaporudi. Yesu hakusema jambo hilo. Yeye alininii tu, kitu Yeye alichosema, “Imekupasaje wewe kama akikaa?” Halafu basi, bila shaka, unasoma katika—katika neno letu, jinsi ambavyo—ambavyo Mungu basi. . . Hilo lilisemwa kwa kusudi fulani. Mambo haya yote ni kwa kusudi fulani. Mungu alimchukua huyo kijana Yohana na kumwinua juu katika Roho, na akaona Kuja Kwake, moja kwa moja mpaka kwenye wa—wakati ujao. Unaona, kasema, “Imekupasaje kama akikaa?” Hakumkawiza, kimwili; bali—bali Neno alilonena kupitia kwake, limetuleta mpaka kwenye wakati huu tulio sasa, unaona. Kwa hiyo, yote yanatenda kazi kwa ajili ya mema.

³⁷ Katika Warumi, mlango unaojulikana sana, ninataka kuchukua vi—vifungu vichache hapa, na vifungu kama viwili ama vitatu vya kwanza, vifungu viwili, nafikiri ndivyo hivyo, na kusoma. Na, katika jambo hili, kujaribu kulielezea hilo vizuri nijuavyo, kwa msaada wa Roho Mtakatifu. Warumi mlango wa 12.

Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu, yenye maana.

³⁸ Nilifikiri fungu hilo lilikuwa ni zuri sana kwa ajili ya kundi hili asubuhi ya leo, kwa yale mliyofanya. Sasa “Wala,” wala ni kiunganishi, ninavyofahamu mimi.

Wala msifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika

mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu.

³⁹ Hivyo ndivyo sisi sote tunavyotaka kufanya, ni, “*Kutoifuatisha namna ya dunia hii, bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zetu, kufanya mapenzi makamilifu na ya kumpendeza Mungu.*” Sasa kwa kuwa tumeokolewa, kama tulivyo; na kwamba tumejazwa na Roho Mtakatifu, kama tulivyojazwa; sasa tunataka nia iliyokuwa ndani ya Kristo, iwe ndani yetu, tupate kugeuzwa kutoka katika mambo ya kawaida ya maisha, na kuletwa ili kufanya mapenzi makamilifu ya Mungu, kwa kugeuzwa, na Roho wa Mungu, kwa Neno Lake.

Sasa somo langu ni: *Nguvu za Kugeuzwa.*

⁴⁰ Ninaweza kuiacha Biblia yangu *hapa*. Sasa, lilikuwa ni jambo la kawaida, miaka kadha iliyopita, wakati nilipokuwa kijana mwanamume kama watu hawa, ha—haikunibidi kuandika Maandiko yangu na—na mambo kadhaa wa kadha wakati nilipokuwa nikisoma. Lakini sasa kwa kuwa ninazeeka, mbona, ninabeba kitabu kidogo. Na—na ninapopata kitu fulani, ati, ninakiandika, inanibidi kukiweka kwenye Maandiko. Na nilizoea ninii, niliukumbuka tu mstari huo wa Maandiko moja kwa moja moyoni mwangu, nilishuka nikaja tu moja kwa moja.

⁴¹ Lakini, enyi marafiki wapendwa, mimi si kijana kama mlivyo ninyi nyote, asubuhi ya leo. Bali mimi ni mzee, nami nimepitia katika vita vingi vigumu, mnaona; na, kwa kupitia katika vita hivyo vikali, kunakuleta mahali ulipo asubuhi ya leo. Unaona? Kwa hiyo, nina hakika mnajua jambo hilo. Mungu amenipitisha katika jambo hilo, kusudi maisha yangu yapate kufungua njia, kusema “Jambo ndilo *hili*, unaona,” ndipo ninyi nyote mnapitia njia hiyo. Lakini mbele yangu, kulikuwa na mtu aliyenifungulia njia niende. Mnaona? Nasi tunafunguliana njia hiyo, mmoja kwa mwingine. Na kama mnavyoona, wakati fulani, shujaa mzee akizeeka, na alama kila mahali mwilini mwake, na kama vile Paulo alivyosema wakati mmoja, “Ninachukua mwilini mwangu chapa Zake Yesu Kristo.” Unaona? Jinsi ambavyo Timotheo aliziangalia chapa hizo, nadhani, kwa uchaji, kama vile alivyomkabidhi kijana Timotheo.

⁴² Sasa, “kugeuza.” Nilikuwa nikifanya kazi katika Kampuni ya Utumishi kwa Umma, ambako tulikuwa na transformia nyingi, na kugeuza. Sasa, hilo neno ni, hilo neno linamaanisha, kwa lenyewe, kitu kama... *Kugeuza*, maana yake ni “kitu ambacho kimebadilishwa, kitu ambacho kimebadilishwa kutoka kitu kimoja kikawa kingine.”

⁴³ Na kama ninavyotaka kusema, kwa dakika zingine arobaini na tano ama saa moja, juu—juu ya huko kugeuzwa, ningependa ku—kutumia kifungu hiki. Na huenda ni—nikasema mambo fulani, kwenye jambo hili, linaloonekana ni la kushangaza sana. Na kama vile Ndugu Leo alivyokuwa amesema hivi punde,

“Lichukue na ulisome tu kwa makini, kwa muda kidogo.” Unaona, liwazie tu kidogo.

⁴⁴ *Kugeuzwa* ni “kubadilishwa na kufanywa kitu fulani tofauti.”

⁴⁵ Kama vile ki—kiluwiluwi, kinageuzwa kutoka kiluwiluwi kikawa chura. Unaona, hapo nyuma, alionekana kama kambare, anaogelea huku na huko, ana—ana kichwa chake na mkia wake, na kila kitu kinaonekana kama tu ka—kambare. Halafu, baada ya kitambo kidogo, anaanza kupoteza, anapoteza mkia wake, naye a—anageuzwa kutoka spishi moja hadi nyingine.

⁴⁶ Hapana budi hilo ndilo nafikiri Paulo alilokuwa akiwazia, hapo aliposema, “Mgeuzwe kwa—kwa kufanywa upya.” Hebu na tuone, hebu nilipate jambo hilo vizuri. “Na msiifuatishie,” mnajua *kufuatisha* ni nini.

... msiifuatishie namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, . . .

⁴⁷ “Kufanywa upya nia zenu.” Mambo yale ambayo mliyawazia wakati fulani, kuwa ni ya thamani, yawekeni hayo kando na mgeuzwe mwe kitu kingine; kile mlichokuwa wakati mmoja, kuwa mlivyo sasa. Mnaona?

... kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu.

⁴⁸ Loo, hivyo ndivyo sote tunavyotaka kujua, jinsi ya kulifanya jambo hilo. Unaona? Tuko hapa, tunampenda; Yeye alituokoa, sasa tunataka kujua la kufanya. Nasi tulikuwa tunajaribu kuchukua hatua kidogo asubuhi ya leo, kuinuka juu zaidi kidogo tu. Mara nyingine inatubidi kugusia mambo ambayo . . . Tulieni tu kwa ninii chache . . . mpaka tutakapoona jambo hili litakavyokuwa.

⁴⁹ Sasa katika Mwanzo, mlango wa kwanza, “Roho ya Mungu ikatulua juu ya uso wa maji.” Tunatambua ya kwamba maji hayo . . . Na—na Biblia ilisema, “Hapo mwanzo kule nyuma,” ya kwamba, hii, “nchi ilikuwa ukiwa, tena utupu.” Hakukuwa na kitu bali giza tupu la machafuko. Na—na hapana shaka ilikuwa katika hali ya kuchukiza sana. Hakukuwa na kitu chochote bali huko mbali kwenye giza, hakuna nuru wala chochote, na mtibuko wa maji, na ile nyota inayohama—hama ilizunguka—zunguka huku na huko kwenye obiti huko nje mahali fulani. Hapana budi ilikuwa ni fu—fungu kubwa mno la—la—la kitu fulani kilichopotea, vile ilivyokuwa, haikuweza kuingia katika njia yake.

⁵⁰ Na hivyo ndivyo tunavyokuwa tunapofanyika nyota zinazotangatanga, mbali na Mungu, bila tumaini kabisa, bila ya Mungu; bila, kuhangaika tu huku na huko, huko katika giza, bila kujua wakati ambapo sisi . . . mahali tunakoelekea.

⁵¹ Ndipo Mungu akauchukua mchafuko huo mkubwa wa giza, na kuubadilisha ukawa bustani ya Edeni, unaona, kwa Neno Lake. Hivyo ndivyo tunavyogeuzwa, kwa Neno la Mungu. Wakati Mungu aliposema, “Na iwe nuru,” na fungu hilo la uumbaji lililopotea huko mbali likaja likaingia na kulizunguka jua, na likanza kulizunguka jua, na likawa bustani ya Edeni kwa sababu lilitii Neno la Mungu. Lilifanya mapenzi makamilifu ya Mungu, kwa kuwa liligeuzwa kutoka kwenye machafuko, likawa bustani ya Edeni kwa Neno la Mungu.

⁵² Sasa hiyo ndiyo sababu ya sisi kuwa hapa. Huo ndio Ujumbe wangu, umekuwa hivyo daima, ni Neno la Mungu. Inatulazimu kulishikilia Hilo haidhuru ni mambo gani mengine yanayotendeka. Dumuni daima na Neno hilo. Daima chunguzeni nia na makusudi yenu, kama ni kulingana na Neno la Mungu. Kama havilingani, acha jambo hilo. Unaona? Lakini kama liko pamoja na Neno la Mungu, na linakubaliana na Neno la Mungu, basi, hilo, wewe lishikilie.

⁵³ Sasa Mungu pengine . . . Kama vile tu kundi lenu dogo hapa asubuhi ya leo. Yeye analiacha jambo lisitukie ghafla, anaacha, Mungu . . . Sisi ndio tunaokuwa na haraka. Mungu kamwe hana haraka. Yeye hulinena tu, na—nalo litatukia. Kwa kuwa, wakati anaposema jambo lolote, halina budi kutukia. Litatukia tu! Yeye, analiacha lichukue wakati wake. Yeye anaacha . . .

⁵⁴ Wale wana wa Kiebrania, hao watu mashuhuri wa Maandiko, waliokuwa wameshikilia kwamba Neno la Mungu ni kweli, walisema, “Mungu wetu anaweza kutukomboza kutoka katika tanuru hili la moto. Hata hivyo, unaona, hatutaisujudia hiyo sanamu, kwa maana ni kinyume cha Neno, unaona. Ingawa, kama Yeye akituua, atatufufua tena, unaona.” Unaona, nao . . . Aliwaacha waende moja kwa moja mpaka ukingoni mwa tanuru hili kubwa, na watumbukie ndani yake, kabla haijaonekana kana kwamba hata alijali chochote, kana kwamba hata hakuwa akiwaangalia. Lakini daima Yeye anaangalia, hata hivyo. Daima anaangalia jambo hili.

⁵⁵ Sasa Mungu alisema, “Iwe nuru.” Na kuwapo kwa Edeni hii kulichukua muda wa miaka elfu sita, nasi tunafundishwa katika Maandiko, “Kwa kuwa siku moja duniani ni . . . ama—ama—ama ni kama miaka elfu, kwa Mungu; miaka elfu moja duniani, ni siku moja kwa Mungu.” Kwa hiyo ilichukua miaka elfu sita kuifanya dunia hii, na kuifanya kuwa Edeni. Lakini, mnaona, ilikuwa ni Mungu, yule Bwana mkuu wa akili zote, Naye—Yeye alijua niani Mwake alichokuwa anataka kufanya.

⁵⁶ Ni kama tu wakati yule mtu aliyetengeneza mkokoteni huu, wakati mtu yule ambaye . . . Wakati ninyi ndugu hapa mliobuni bustani hii, jinsi ambavyo mngaitengeneza, ilikuwa niani mwenu, mlidumu kulifanyia kazi ono hilo.

⁵⁷ Hivyo ndivyo Mungu alivyofanya kuhusu dunia. Alifanya kazi; ilikuwa niani Mwake. Na, kama ukiangalia, ilitokea kwa mageuko, kana kwamba alikuwa akiendelea kujifunza daima mambo ya zaidi, akiendelea kufanya kitu fulani bora zaidi na zaidi. Lakini, unaona, Yeye alikuwa juu ya yote, naye akayaacha tu yageuke kufikia kiwango hicho, unaona. Kila kitu alichianza kuleta juu ya nchi, kuanzia katika maisha ya mimea, na samaki, na kadhalika; ikafikia kwenye ndege, na wanyama; na halafu kitu fulani katika sura Yake Mwenyewe, mwanadamu; ndipo akakomea hapo, unaona, kwa maana ilikuwa imefikia ukamilifu Wake, wa kile alichokuwa anataka.

⁵⁸ Hivyo ndivyo unavyoanza, kama mkokoteni huu. Penguin unaunda fremu yake, na useme, “Unafanya nini?” Kama vile ninyi, wakati ninyi nyote mliposogeza mawe ya kwanza kutoka hapa pembeni. “Mnafanya nini?” Unaona, haikuonekana kana kwamba ingekuwa kama jinsi ilivyo sasa. Inaonekana kama Edeni ndogo, kwa maana mlikuwa mnajua la kufanya mawazoni mwenu, nanyi mliendelea tu kutenda kazi.

⁵⁹ Sasa tunataka kugeuzwa, sisi wenyewe, kwa kufanywa upya nia yetu. Unaona, si yale tuliyo nayo humu duniani, yale tutakayotafuta humu duniani; bali ni yale tunayoyaendea, katika ulimwengu ujao. Kugeuzwa kwa kufanywa upya nia yetu!

⁶⁰ Sasa, miaka elfu sita, Mungu alichukua kuufanya huu, na tunaona katika Mwanzo 1. Hata hivyo, sasa tunaona ya kwamba, katika jambo hili, Mungu alikuwa na ninii—alikuwa na kusudi alilotaka kutimiza.

⁶¹ Na watu wengi sana, katika kufundisha juu ya Mwanzo, huku nyuma katika mlango wa kwanza na mlango wa pili, na mlango wa 3, hasa, “Inaonekana kana kwamba Mungu anajirudia Mwenyewe, au Yeye alisema, aliendelea na kusema mambo haya yote aliyofanya. Loo, jinsi ambavyo Yeye... ‘Iwe nuru, na *hiki* kiweko, na kutokee,’ wala hapakuwa na kitu hata kimoja bado.” Hakukuwa na chochote. Hakukuwa na nuru. Ulimwengu hu—huo wa kale ulikuwa ungali unaelea mbali huko katika giza hilo, umefunikwa na maji. Lakini, unaona, Yeye alikuwa ametamka Neno Lake, halafu basi hapo ndipo alipokuwa akinena.

⁶² Sasa tunaona hapa katika Mwanzo 1, Yeye alisema, “Naye alimfanya mtu katika mfano Wake Mwenyewe, katika sura Yake Mwenyewe, alimfanya (Yeye alimfanya) katika mfano wa Mungu, mwanamume na mwanamke.” Unaona, Yeye alikuwa akimfanya mwanadamu, alinena Neno tu. Ndipo tunaona, baada ya siku Zake nyingi kupita, labda mamia na mamia ya miaka, kungali hakukuwa na mtu wa kuilima ardhi. Hakuna mtu wa kuilima ardhi, kwa hiyo basi Mungu akamfanya mtu kutoka katika mavumbi ya nchi. Unaona, Yeye alikuwa amenena Neno, na ndipo ilibidi Neno litimie.

⁶³ Sasa, wakati aliposema, “Iwe Nuru,” labda huenda kulikuwa na mamia ya miaka, labda miaka mia nane, kabla hata hakujakuwa na nuru, bali ilikuja kutimia kwa maana Mungu alisema hivyo.

⁶⁴ Na Mungu atakuwa na Kanisa, sijali tutapitia kwenye nyakati za giza ngapi, na kadhalika. Yeye atakuwa na Kanisa lisilo na waa wala kunyanzi, kama sisi ni sehemu yake ama la, kwa maana tayari amekwisha kusema itatukia. Litakuwako.

⁶⁵ Na—naye aliamuru, ku—kuigeuza iwe na uhai wa mimea na kila uhai aliouweka. Yeye alisema maneno haya, kama, “Na kuwe na mtende. Kuwe na mwaloni. Kuwe na msonobari.”

⁶⁶ Angalia kule chini jangwani, mahali tunapoishi hapa Tucson. Huko nje, kuna mpungate, mpungate urukao, kila aina ya mipungate. Dakika thelathini tu kutoka hapo, ni msonobari wa Sherman huko juu ya mlima. Sasa, mpungate huu hautamea *kule* juu, na wala huo msonobari wa Sherman hautakua *huku* chini. Sasa, ile Akili iliyoipanda hiyo mbegu ilikuwa wapi? Unaona, ilibidi zije toka mahali fulani. Ilikuwa ni Neno la Mungu, “Na iwe,” na ikawa.

⁶⁷ Sasa tunaona, yote haya, (baada ya kuifanya, kuigeuza ikawa kwa jinsi yake na kwa uhai wa aina yake, na—na vyote viliwekwa humo kwa Neno la Mungu, Muumba), Yote hayo, tunaona, ya kwamba haya yote yalielekea kwenye makao makuu, yaliyoitwa bustani ya Edeni. Na Mungu alimweka mwanawe, na bibi-arusi wa mwanawe, juu ya yote hayo. Unaona? Uumbaji huu mkuu, unaona, Yeye alikuwa na sababu kwa ajili ya hilo. Yeye alifanya kila kitu kuwa kizuri sana! Alifanya maua, na uhai, na ndege; wala hakukuwa na mauti, wala dhambi, wala huzuni, wala maradhi. Na ndipo kitu hiki chote kikuu kilielekea kwenye makao makuu, ambayo yalikuwa ni bustani ya Edeni.

⁶⁸ Na hapo akamweka mwanawe, Adamu, na bibi-arusi wa Adamu, mkewe. Sasa pengine ungesema, “Ilikuwa ni mkewe.” Kwa kukusudiwa ilikuwa ni mkewe, bali kamwe hakuwa... bado hakuwa hasa amepata kuwa mkewe.

⁶⁹ Kama vile katika Maandiko, tunaona, mahali yaliposema, “Yusufu, mwana wa Daudi, usihofu kumchukua Mariamu mkeo, kwa maana mimba yake ni kwa uweza wa Roho Mtakatifu.” Unaona? Sasa alikuwa ni mke wake wakati alipotoa ahadi ya kumwoa, ama kumchukua; bali hata hivyo hakuwa ni mkewe, bado, kwa sababu hakuwa amemjua kama mke.

⁷⁰ Kwa hiyo hivyo ndivyo jinsi ilivyokuwa hapa, sababu ya mimi kusema, “Mwana wa Mungu na bibi-arusi wake.” Adamu hakuwa kamwe amemjua mke wake kama mke, lakini hata hivyo alikuwa ni mke wake, kwa kukusudiwa. Kama vile tu kanisa sasa, na Kristo.

⁷¹ Sasa, basi, yote yangeweza kutulia, kwa kuwa mbegu zote za Neno zuri la Mungu, alizokuwa amezinena, zilikwisha za

kwa jinsi yake. Dunia ikageuka upande mwingine, kukawa na nuru. Kulikuwa na nuru ya jua wakati alipoliacha jua liwake. Sasa kwa nini alilifanya jua liwake? Yeye alikuwa amekusudia niani Mwake, unaona, kwamba, jua lisipowaka, ua halitaota, ambalo alinena likawepo. Yeye anafanya kila kitu kutimiza kusudi lake, chochote kile. Kama vile mti, unazaa aina fulani ya tunda la muoka, ama unazaa tofaa. Yeye huumba tunda la shamba, na kadhalika. Yote ni kwa kusudi Lake. Na kila kitu kilitimia, Naye alikuwa amekwisha nena jambo hilo. Sasa jambo pekee lililompasa kufanya, baada ya kunena jambo hilo, Yeye... akilineni, vile ilivyokuwa hasa. Yeye aliweza kwenda kupumzika, kwa kuwa alikuwa amekwisha kulinena, na ilikuwa yote yatimie kwa sababu alikwisha nena jambo hilo. Sijui lilipaswa kupitia kwenye mambo mangapi kabla halijatimia, kwamba lilikataliwa mara ngapi na kadhalika. Bali lilipaswa kutimia, kwa kuwa alisema lingetimia. Alikuwa amelinena.

⁷² Jambo lile lile ndivyo lilivyo kuhusu kuwa na Kanisa hapa katika siku za mwisho. Yeye atakuwa na Bibi-arusi. “Yeye anaweza kutoka katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto.” Kama hatumfuati, Yeye atamchukua mtu mwingine ambaye atamfuata. Unaona? Yeye atakuwa Nalo, kwa kuwa tayari amelinena. Lolote asemalo, halina budi kuwa hivyo. Haliwezi kubadilika. Halina budi kutokea namna hiyo, kwa kuwa alisema litakuwa hivyo alivyonena.

⁷³ Na jambo hili lote kubwa ambalo alijua lingetimia, baada ya Yeye—Yeye kulinena, aliweza kupumzika. Kila kitu kimetawaliwa! Mbegu Yake ilikuwa ni Neno Lake, na Neno Lake ni mbegu. Yesu alisema lilikuwa ni mbegu. Na kila kitu kingekuwa sawa, kwa maana alikuwa amekwisha kusema ya kwamba lizae la aina yake, likigeuzwa kuwa la jinsi yake tu. Unaona, ilibidi Neno Lake liwe la jinsi Yake. Kama alisema “mtende,” hakumaanisha mchanganyiko wa mtende na mwaloni. Alimaanisha mtende *hapa*, na *mwaloni* hapa, kila kitu kuwa katika mahali pake.

⁷⁴ Loo, laiti tungaliweza tu kujifunza hayo, ya kwamba sisi tu sehemu gani ya Neno, yatulazimu kusimama kwenye nafasi yetu, haidhuru iwe ni nafasi gani.

⁷⁵ Ninamfikiria dada fulani mdogo hapa kwenye kiti cha magurudumu, wakati fulani, kwamba ni sala ngapi za uaminifu zimefanywa juu yake. Basi hatufahamu, kwa hiyo tunalikabidhi tu kwa Mungu. Na... yeye ni ua hapa miongoni mwenu, pamoja na kufurahisha kwake na kila kitu. Unaona, ni kwamba sisi tunaweza kuamka na kwenda huku na huko, jinsi ambavyo angetaka kufanya jambo hilo, lakini hata hivyo yeye anafurahisha tu jinsi anavyoketi. Daima ninavuviwa kumwanguka maskini bibi huyo, unaona, kwa maana yeye... Sote tutaamini katika uponyaji. Tumemwona Mungu akifanya miujiza mikubwa mno zaidi ya hiyo, unaona. Na bibi huyo

anajua jambo hilo, pia, unaona, bali yeye yuko tayari kusimama kwenye nafasi yake.

⁷⁶ Unaona, chochote kile, hivyo ndivyo tunavyotaka. Nami ninaamini ilikuwa ni Daudi, aliyesema, “Afadhali niwe jamvi mlangoni mwa nyumba ya Bwana, kuliko kuishi katika hema pamoja na waovu.” Unaona, haidhuru ni nini, “nitasimama kwenye nafasi yangu.”

⁷⁷ Mara nyingine inakubidi kujitenga na kila kitu unachokipenda wewe, duniani, upate kuchukua nafasi yako ambayo Mungu amekuitia. Nina hakika unaweza kusoma katikati ya mistari, yale ninayosema. Unaona? Wakati mwingine mtu unayempenda kuliko wote duniani, inakubidi kuagana nao; na uchukue nafasi yako katika Kristo, ufikie mahali ambapo Mungu amekuitia. Unaona? Lakini Mungu anafanya jambo gani? Anakugeza kutoka jinsi ulivyokuwa. Pengine wewe ni binti ama mwana, ama chochote kile, kutoka katika familia nzuri wakati mwingine, Yeye hukuweka mahali pengine. Kwa sababu, hiyo ndiyo njia Yake ya kufanya jambo hilo, unaona, kwa kufanywa upya nia yako, ili kutii Neno la Mungu, haidhuru itagharimu kitu gani. Unaona? Mambo haya hayaji. . . Hayakutokana. . .

⁷⁸ Ukombozi wetu haukuwa ni jambo rahisi, ilimpasa Mwana wa Mungu kufa kwa ajili yetu. Unaona? Si ninii. . .Vitu vya thamani hugharimu gharama kubwa.

⁷⁹ Kuuleta Ujumbe huu, haikuwa rahisi. Unaona? La, si rahisi. Ilinibidi kuacha kila kitu nilichokipenda, hata familia yangu mwenyewe, kila mtu. Lakini mnaona thamani yake ni nini, mnaona, ni kufanya mapenzi ya Mungu. Na ili kufanya jambo hilo, ambalo ninajua kuna kitu fulani ndani yangu, wakati walipokuwa wakisema. . .Vema, wanaenda kunitupilia mbali; walidhani nilikuwa nimechanganyikiwa. “Nikibatiza katika Jina la Yesu Kristo, kinyume na kanisa. Na mambo haya yote!” Wao walisema, “Yeye ni mwenda wazimu.” Lakini, unaona, haidhuru walisema nini, kuna jambo fulani linalopaswa kufanywa. Na Mungu humchukua tu mtu fulani, anamshika mkononi Mwake, na kusema, “Fanya hivi,” na unalifanya.

⁸⁰ Huenda ilikuwa ni gharama ya jinsi gani kwa Mtakatifu Paulo; aliyefunzwa chini ya Gamalieli, mwalimu aliyekuwa mashuhuri sana kuliko wote wa siku hiyo. Na kushuka chini, na jambo lile lile alilolifikiria kwamba ni uzushi, mambo aliyodhania ya kwamba yalikuwa ni mabaya zaidi ambayo yangeweza kutukia kwa kanisa, anayajia moja kwa moja na kuwa mshiriki wa hayo. Jambo la ajabu! “Na jinsi Mungu anavyotenda kazi katika njia za kushangaza, katika njia za ajabu, za kipekee, kutenda maaajabu Yake.”

⁸¹ Wakati Mungu alipokuwa amenena jambo hilo, Yeye alijua Neno Lake lilikuwa ni mbegu; na lingeweza, lingezaa kwa jinsi

yake. Sasa, mbegu iliamriwa kuzaa tu kwa jinsi yake, na daima itafanya hivyo kama mwanadamu hataichezea.

⁸² Na vivyo hivyo Kanisa la Mungu na chochote kile, kitazaa kwa jinsi yake kama ile ilivyokuwa kwanza, kama wanathiolojia wasingelicheza-cheza na Neno hilo, wakijaribu kuliweka mahali pengine, ama kuingiza kitu kingine. Mungu amelinena. Na haidhuru wanaweza kufanya hivyo jinsi gani, wanavyojaribu kulichafua na kulichezea, na kadhalika, litazaa kwa jinsi Yake. Hakuna kabisa kitu chochote cha kulikomesha.

⁸³ Natumaini sisikiki kana kwamba ninawapigia makelele ninyi nyote. [Ndugu Branham anarekebisha maikrofoni—Mh.] Je! sauti hiyo ni kubwa mno? [Kusanyiko linasema, “La.”]

⁸⁴ Basi, angalia, sasa tunaona kila kitu kiko katika utaratibu. Mungu alikinena, Naye alisema, “Na iwe, na iwe. Na Edeni iwepo. Kuwe na maua mazuri. Na mwanangu awepo, katika mfano Wangu, asimame pale katika bustani ya Edeni, na hebu bibi-arusi wake asimame karibu naye.” Loo, linapendeza jinsi gani, jinsi hilo lilivyokuwa. Naye Baba, Yeye alikuwa ni Baba, unaona, kwa hiyo watoto Wake Mwenyewe wakatokea wakaja. Naye akawatengenezea paradiso. Mungu anapenda kuwafanyia watoto Wake mambo.

⁸⁵ Hivi hamkumbuki jinsi ambavyo, ninyi akina mama, na jinsi ambavyo haidhuru jinsi gani; kama ingaliwabidi kupunguza posho mezani, kama Kadogoo alihitaji jozi nzuri ya viatu ambavyo alivipenda, u—ungefanya jambo hilo, unaona. Chochote kile, kuwafanyia watoto wenu jambo fulani! Baba, jinsi ambavyo ungefanya kazi kwa bidii zaidi, upate kitu fulani cha kuwapa watoto. Unaona?

⁸⁶ Vema, hiyo inaonyesha tu ya kwamba tuko hapa *chini* kabisa, mzazi. Yeye ndiye Mzazi halisi, unaona, na ni zaidi sana kiasi gani! Si ajabu yule mtume alisema, “Jicho halikuyaona, wala sikio halikuyasikia, wala hayakuingia katika moyo wa mwanadamu, mambo ambayo Mungu amewawekea, amewaandalia, wampendao.” Hatuwezi kamwe kuwazia niani mwetu, sisi, akili yetu haifai kuwazia kuelekea kwenye mwelekeo hali—halisi wa mambo yale ambayo Mungu ametuandalia, kwetu sisi tunaompenda. Mnaona, sisi, ninaweza kuwazia jinsi itakavyokuwa, ninaweza kufikiria jinsi itakavyokuwa, bali si—si...akili yangu ha—ha—haina uwezo wa kuwazia jinsi yalivyo makuu. Kwangu hayawaziki. Je! unaweza kuwazia jinsi Mbinguni kutakavyokuwa wakati sisi sote tutakapokuwa kule, na tukiwa vijana, wala hakuna dhambi? Wala hakuna...Loo, ni mahali pazuri jinsi gani! Lakini, unaona, ni zaidi ya hayo. Unaona, sisi, “hata haliwezi kuingia katika moyo wa mwanadamu, yale ambayo Mungu amewawekea, amewaandalia.” Yeye alianena, na yatatukia.

⁸⁷ Sasa baada ya mpangilio huu wote mzuri aliokuwa nao pale, wa ninii Yake...Simaanishi kulisema hilo kwa neno hilo, mpangilio, lakini kwa namna fulani ni kama ninii...Hivi mama, kabla ya kuzaliwa mtoto, hivi seti hiyo ya mahitaji ya mtoto mchanga hawaiti hivyo? Wanaandaa ninii...vijiatu vyote vidogo na kila kitu vinawekwa tayari, unajua, kwa ajili tu ya kuwasili kwa sehemu hii ndogo ya upendo ambayo Mungu anatumia, kuvitayarisha hivyo.

⁸⁸ Hivyo ndivyo Mungu alivyowafanyia Adamu na Hawa. Yeye aliumba bustani hii ya Edeni. Alikwishainena, ilikuwa katika nia Yake. Na anapotamka kitu, basi hakina budi kutukia.

⁸⁹ Zingatia jambo hilo niani sasa. Kile Yeye asemacho, hakina budi kutimia! Unaona, na Yeye hawezi...Hakuna kitu kinachoweza—kinachoweza kukizua, hakuna kitu kinachoweza kukizua kisitendeke. Hakuna kitu kinachoweza kukizua kisitukie. Mungu alisema hivyo, hilo latosha! Mungu alisema hivyo, litatukia.

⁹⁰ Sasa yeye aliwazia haya yote, Naye akasema, “Na iwe.” Sasa, hiyo ni Mwanzo 1, unaona, “Na kuwe *hiki*. Na kuwe *kile*. Na kuwe.” Alikuwa akipanda mbegu. “Na kiwe *hapa*. Na kiwe *hapa*. Na kiwe *hapa*.” Naye alijua itakuwa hivyo, kwa kuwa haiwezi kubadilika.

⁹¹ Sasa hilo linatupa imani, basi. Na kile alichosema *Hapa*, kitakuwa. Kwa hiyo hebu na turuhusu Mbegu hiyo ianguke mioyoni mwetu, ili tupate kuwa tuta la kuoteshea la Hiyo, unaona, mioyoni mwetu. Na hebu na tuicheze nafasi hii ambayo Yeye alituweka ndani yake, katika siku za mwisho. Unaona, “Jalia hiyo Mbegu ianguke ndani ya mioyo yetu, Bwana. Jalia Neno Lako lianguke ndani ya moyo wangu.” Jalia kusiwe na kutokuamini kokote!

⁹² Kama Ibrahimu, wakati alipokuwa mzee, ilionekana kana kwamba haiwezekani. “Wataendaje kufanya jambo hilo? Yeye ataendaje kuwa namna hii?” Hakuwazia jambo hilo. Alilipokea tu Neno la Mungu, na akaendelea kuliamini, naye Mungu akalitimiza. Sasa, Mungu alikuwa ameyanena mambo yote haya, kwa hiyo alijua yatakuwa. Nayo yakawa, Yeye aliyaleta hayo kwa jinsi yake.

⁹³ Sasa kwa kuwa Yeye alikuwa amegeuza basi, mbegu hizo zote zikawa kiumbe hai na uumbaji uliipaswa kuwa, vilitokea tu kwa jinsi Yeye alivyosema vingetokea. Au, Yeye alisema, “Na iwe.” Labda mamia na mamia ya miaka yalipita, lakini hapa tunaona Edeni inayopendeza, na ndege wakubwa wakiruka. Hao ndege hawakuwa wafe. Na mbwa mwitu na mwana-kondoo walikuwa wakila pamoja, na simba, chui na maksai. Wala hapakuwa na mauaji, wala mauti, wala huzuni. Na kulikuwa na Adamu na Hawa, wakitembea katika bustani ya Edeni. Kila mbegu ikizaa, isingeweza kufanya jambo lingine lolote kamwe.

Isingeweza kufanya kitu kingine chochote, kwa sababu Mungu alisema, “Na iwe hivyo ilivyo.” Ilibidi iwe namna hiyo.

⁹⁴ Loo, jinsi ambavyo ningependa kusimama hapa kwa muda kidogo tu, kusema, unaona, huko ndiko tunakoelekea, hata hivyo, kule kukamilishwa kwa Neno.

⁹⁵ Sasa Mungu alisema, “Na iwe.” Na hapa ikawa, kwanza, kikamilifu, vivyo hivyo kabisa. Sasa, mti *huu* unaweza tu kuzaa mti ule. Mti *huu* unaweza tu kuzaa mti huu. Naye Adamu, mwana wa Mungu, anaweza tu kuzaa mwana wa Mungu. Unaona, mnapata ninalomaanisha? Ni kila kitu kwa jinsi yake, na kwa hiyo Mungu angeweza kusema, “Vema, nitapumzika tu sasa.”

⁹⁶ Na hivi ulijua, yalikuwa ni maneno machache sana Mungu aliyopata kunena, kwa kweli, tangu wakati huo na kuendelea? Yeye alikabidhi jukumu hilo, baada ya kule kuanguka, kwa manabii Wake, nao wanalileta Neno sasa, unaona. Mungu alistarehe, hakuwa na lolote la kufanya tena. Wanaenda tu kwenye makao Yake makuu na kubisha mlangoni na kusema, “Baba, ni kitu gani?” Naye analituma chini Neno akiwatumia wao. Unaona, Yeye ana mfumo, na namna ya kufanya mambo hayo.

⁹⁷ “Hebu na iwe tu. . .” Na hivyo ndivyo ilivyokuwa, kila kitu, kwa mbegu ya jinsi yake ikizaa kwa jinsi yake. Sasa wakati kila kitu kilipoonekana ni kizuri sana, na kila kitu kikienda kutimia kama vile tu Mungu alivyokuwa amesema, sasa huyu hapa yule mjanja mdanganyifu, mchafu anakuja.

⁹⁸ Sasa hilo ndilo ninalojaribu kuwaonya nalo ninyi nyote hapa kulihusu. Mnapoona Mbegu ya Mungu ikianza kushikilia, kukua, mwangalie jamaa huyo akiingia kwa ujanja tu kadiri awezavyo, akimnukulia Maandiko vizuri yule ambaye asingekuwa nayo, unaona. Mwangalie, maana yeye ni mdanganyifu.

⁹⁹ Nitaliita, badala ya mge—mgeuzi, kugeuzwa, yeye ni mharibifu, anaharibu mambo ambayo yamegeuzwa kuwa mazuri. Yeye ni mharibifu, na, yeye, mharibifu, ama mpotoshaji ama mchafuzi wa Mbegu ya asili na mpango wa asili.

¹⁰⁰ Sasa mnaona hapa, kama vile katika kundi lenu hapa asubuhi ya leo, mna mpango, mna ono. Sasa mwangalieni huyo mpotoshaji, loo, yeye atakuwa mjanja na mwerevu awezavyo kuwa, unaona. Lakini shikilieni ono lenu, jamani. Unaona, endeleeni kushikilia hilo.

¹⁰¹ Sasa pia tunaona ya kwamba, wakati alipoingia, yeye aliiharibu mbegu hiyo. Na akaipotosha mbegu hiyo kwa kuingia kwenye tuta la uzazi, ambalo lilikuwa ni Hawa, na kuipotosha mbegu hiyo, kwa mbegu ya upotovu, kabla haijafika pale, kuipotosha hiyo bustani nzuri ya Edeni.

¹⁰² Ambapo—ambapo, Mbinguni, jambo pekee lililopo, ni kurudishwa tu. Mahali tulipo sasa, tuko njiani tukirudi kwenye ule mwanzo wa asili wa uumbaji wa Mungu, kurudi kwenye bustani ya Edeni tena; mume na mke, bila—bila ninii yoyote—dhambi yoyote wala chochote kile, kuishi Milele. Lakini kule—kule kuge...kule...

¹⁰³ Sasa, sasa Yeye anatutaka sisi tugeuze nia zetu, kwa kufanywa upya; ama tuwe tumegeuzwa, kugeuzwa kwa kufanywa upya nia ze—zetu.

¹⁰⁴ Sasa Shetani anaingia na anaingiza kitu cha kuliharibu Neno, akilifanya liseme kitu ambacho sicho. Sasa hivyo ndivyo alivyofanya pale mwanzo. Na sasa angalia, hili litasikika kuwa ni la kushangaza sana asubuhi ya leo, kwa—kwa watu, kama sitangoja na kuweka mawazo mengi sana hapa kabla sijafikia wazo langu la kawaida nililotaka ku—kuwaletea. Ni hili, ya kwamba, yule mvurugaji aliingia; na kama vile ambavyo Mungu alichukua miaka elfu sita na Neno la asili, kuleta kila neno kwa jinsi yake, na kila kitu ambacho alifanya kingekuwa ni Neno la Mungu Mwenyewe likizaa kwa jinsi yake, sasa huyo mwenye kuharibu amechukua miaka elfu sita, na kulivuruga Neno hilo la Mungu. Na je! yeye amefanya nini? Amejiletea Edeni mpya, Edeni ya Shetani. Humo ndimo tunamoishi leo.

¹⁰⁵ Yeye alifanyaje jambo hilo? Lingetukiaje? Sasa sehemu ya kushangaza ni jinsi alivyofanya jambo hilo. Na hapo ndipo ambapo inatubidi kuninii, sababu ya mimi kuwa hapa, kuyatoa haya mbele zenu, ili kwamba mweze sasa kuyasoma, na pamoja na hawa ndugu hapa, na wengineo, katika majuma yajayo, mpate kuona jinsi vile Shetani alivyofanya jambo hili. Pia angalieni jinsi alivyo mjanja, na jinsi alivyo mdanganyifu.

¹⁰⁶ Sasa, yeye aliziharibu mbegu hizi. Sasa, yeye asingeweza kuziangamiza, aliziharibu. Sasa tunatambua ya kwamba dhambi ni haki iliyopotoshwa. Ni kwamba tu uongo ni kweli iliyowakilishwa vibaya. Unaona, na vivyo hivyo kitu chochote. Uzinzi ni tendo sahihi, ambalo Mungu aliliruhusu, lililotendwa tu kwa njia mbaya. Unaona, na vivyo hivyo kitu chochote. Na mauti ni upotovu wa uhai. Mauti yanachukua tu, unaona, yanaharibu uhai.

¹⁰⁷ Sasa alikuwa na miaka elfu sita ya kufanya jambo hilo kwa manyunyu yake ya sumu. Na yeye alifanyaje jambo hilo? Sasa hii ndiyo sehemu ya kushangaza sana. Na sikilizeni kwa makini sasa. Yeye alifanya hivyo kwa ustaarabu. Sasa hilo linasikika la kushangaza, lakini ndivyo hivyo. Nitatoa tamshi hapa ambalo litawafanya mwendelee kutafakari, labda, kwa dakika chache; natumaini sivyo. Lakini je! mlitambua jambo hili? Sasa mimi sijaribu kuunga mkono ujinga. Lakini je! mlijuu ya kwamba ustaarabu, sayansi, elimu, na mambo ambayo tunayapenda sana leo, ndiyo chombo cheneyewe hasa cha Shetani, yaani ustaarabu? Ustaarabu kamwe haukuletwa na Mungu. Ustaarabu uliletwa na

Shetani. Sasa nitawathibitishia jambo hilo kwa Neno, mnamo dakika chache tu.

¹⁰⁸ Ustaarabu si wa Mungu. Kwa kuwa, hebu niwaonyeshe; katika ustaarabu huu, kadiri tunavyostaarabika tunapofanya kazi kwa sayansi, daima tunajiua wenyewe. Unaona? Na ustaarabu huu umejiunga kufikia kwenye kilele chake sasa, nasi tuna mauti katika ustaarabu huu. Tuna dhambi katika ustaarabu huu. Tuna magonjwa katika ustaarabu huu. Huo hauwezi kuwa ni wa Mungu.

¹⁰⁹ Kwa hiyo, Mungu, katika ule Uta-...Ufalme Wake Mwenyewe mkuu utakaokuja, tutakuwa na ustaarabu, bali hautakuwa ni kitu chochote kama huu. Hautakuwa kwa sayansi. Utakuwa ni ustaarabu wa imani, kwa Neno. Unaona?

¹¹⁰ Ustaarabu huu wa kisayansi tulio nao, ni mtego halisi wa Shetani, na huo ndio ambao amewaua watu nao. Huo ndio anaotua nao, kila siku. Hivyo ndivyo ambavyo, tunapokula, kila siku; badala ya kuishi, tunakufa. Wamepotosha sana kila kitu, hata wanachukua tu kiasi kadhaa cha *hiki* na kukichanganya na *hiki*, na kuzalisha *hiki* na *kile, kile*, mpaka kinakufa. Ni jamii inayokufa. Na haidhuru unajaribu kufanya jambo gani, unakufa.

¹¹¹ Mliona ile sinema jana usiku, ya hao Waafrika. Unajua ni kwa nini? Hao kamwe hawajatumia penisilini. Hao watu wanaishi muda mrefu zaidi kuliko tunavyoishi. Wao hata hawajui wananinii...Viini vya maradhi haviwasumbui. Unaona, mbona, kiini kingeinua mkono wake na kujisalimisha kwao. Unaona? Kwa sababu yeye, unaona, yeye haninii, yeye... Wao hawaninii. Kwa nini? Hawakuninii kabisa...Unaona, sisi tutachukua, sayansi kulitatua, kama vile penisilini ama kitu fulani watakachoweka ndani yetu, ku—kuondoa ugonjwa huu, na hicho kinararua kitu kingine, na kufanya tuta la kusia kwa ajili ya kitu kingine. Unaona? Sasa, yeye hafanyi jambo hilo. Unaona?

¹¹² Sasa yeyote, wengi wenu ninyi watu mnatoka mashambani. Mtu yeyote anajua ya kwamba mmea mzuri wenye afya hauhitaji kunyunyiziwa kamwe. Una—una kinga ndani yake, ya uhai, kwamba mdudu hata hataweza kuuandama, kwenye mmea halisi—kwenye mmea wenye afya ya kweli. Ni mmea huu wa tuta lenye samadi, mmea huu chotara, ndio unaokubidi kuubembeleza!

¹¹³ Kwa mfano, baadhi yenu ninyi jamaa hapa ni watu wa Magharibi hapa. Angalieni huko nyuma katika ule wakati wa ng'ombe mwenye pembe ndefu. Siku hizi mnasema mna nyama bora zaidi na ninii wenu—ya Hereford wenu. Ati mna nyama bora? Hamna. Ng'ombe huyo mwenye pembe ndefu, si kwamba ninamtetea ng'ombe huyo, bali angeweza, angeweza kukaa hapa

nje kwenye msimu wa baridi kali kama ayala. Loo, alikuwa amekonda sana na kila kitu, lakini alikuwa ni maradufu . . .

¹¹⁴ Huyu Hereford, mnamwekea nyasi kavu chini yake, mnapompiga picha, kufikia karibu kwenye tumbo lake, kuonyesha ya kwamba yeye ndiye nyama kwa goti la mguu wa nyuma. Na ni kitu gani? Hebu mfungulie umwachilie huko nje, angekufa. Asingeweza kustahilimili majira ya baridi kali hata akifanya nini. Inakubidi kumlisha, na chochote kile, kumshughulikia, kumbembebeza kwa kila kitu. Yeye ni chotara. Unaona? Lakini yule ngombe halisi mwenye pembe ndefu, mwachilie tu.

¹¹⁵ Hivyo ndivyo ilivyo siku hizi na Wakristo wetu. Tuna wengi sana inaotulazimu kuwabembebeza, kuwasihi, kuwaweka ninii, kuwafanya shemasi kanisani, kuwapigapiga mgongoni, na kumpa mtu cheo kikubwa sana kanisani. Ama, usipofanya hivyo, mbona, yeye, hataninii—hataingia, kama usipomwacha *huyu* afanye jambo hili, na *huyu* afanye vile. Ni kuwabembebeza.

¹¹⁶ Ungeweza kuwazia Wakristo halisi wakiwa hivyo? Walikuwa washupavu. Walikuwa wajasiri. Ungemwazia Mtakatifu Paulo kuwa ni Mkristo wa aina hiyo, ungeweza kumwazia Mtakatifu Petro, “Kwa kuwa sasa—sasa, msiponifanya kiongozi mkuu, vema, sijui, huenda nikaenda na kujiunga na *Fulani*”? Walikuwa ni watu wasiotaka mchezo. Walikuwa ni watu wa imani. Walidumu na Mungu. Walitembea pamoja na Mungu. Walikuwa ni watu wa maneno machache. Walimtumikia Mungu, mchana na usiku, daima. Hakikulazimu kuwanyunyizia na kuwabembebeza, na kuwahonga *hiki*, *kile* ama *kinginecho*. Walikuwa ni wanaume, wagumu! Walikuwa ni mbegu halisi, si machotara katika madhehebu.

¹¹⁷ “Ikiwa ninyi, Wamethodisti hamtanitendea ipasavyo, nitaenda kwa Wabaptisti. Wabaptisti wasiponitendea vyema, nitaenda kwa Wapentekoste. Kama hawatanitendea vyema, nitarudi kwa Wakatoliki, ama kwa wowote wale.” Unaona, wao, ni chotara, huna budi kuendelea kuwanyunyizia ukiwanyunyizia, “Naam, Daktari Kasisi Ndugu *Fulani*.” Huo si Ukristo.

¹¹⁸ Ukristo unaomba—hauombi wadhifa wo wote, hauombi upendeleo. Unamjua Mungu tu. Ni mbegu ya asili. Unampenda Mungu, na hupendana mmoja kwa mwingine. Hakuna kuwanyunyizia, na kuwabembebeza, na kuwatuliza, na kusema, “Naam, vema, dada *huyu*, vema, ninafikiri ni sawa kwake kuwa na nywele fupi, na *huyu* asiwe nazo.” Na—na hakuna kitu kama hicho, na kuwaachilia waendeleo na jambo *hili*. Ni—ni rafu, ni Injili! Hebu isambaze huko nje, acha ianguke mahali popote. Wakristo wanaipenda.

Hivi ni lazima nibebwe Nyumbani, Mbinguni,
Kwenye kitanda cha raha cha maua,
Wakati wengine walipigana wapate kushinda
tunzo

Na wakaabiri katika bahari zilizojaa damu?

119 Hivi inabidi nipigwepigwe mgongoni, na *hivi, vile*, na *vinginevyo*, na kubembelezwā? Ninatarajia mahali pangu huko ng'ambo pamoja na walio washupavu. Sitarajii kuja huko juu bila makovu ya tunzo hata kidogo.

Kama inanibidi kupigana, kama inanibidi
kutawala, ongeza ujasiri wangu, Bwana!

120 Unaona, hebu nisimame kama Mkristo. Sio niwe m—mmea chotara. Unaopaswa kubembelezwā na kudekezwadekezwā, na kuingizwa ndani ya kitu fulani. Huingizwi vivi hivi, Ukristo, unazaliwa ndani yake. Unakuwa kiumbe kipya, wewe ni mbegu ya Mungu, inayokuja duniani.

121 Sasa, sasa tunaona ya kwamba yeye alinyunyiza manyunyu haya ya sumu, na manyunyu hayo yalikuwa ni manyunyu ya maarifa ya kisasa, elimu, sayansi, na ustaarabu, vitu vile hasa tunavyopenda sana. Je! ulipata kutulia na kuwazia ya kwamba adui yetu mkuu, katika maisha ya kawaida leo miongoni mwa mataifa, ni ukomunisti? Mungu wa ukomunisti ni nini? Ustaarabu, na elimu, sayansi. Hiyo ni kweli, sivyo? Hayo ndiyo wanayoishi kwayo na kustawi kwayo, ni sayansi, ya kisayansi, sayansi mbalimbali, mungu wa sayansi. Sasa kama mngeninii tu... na kwa manyunyu ya sumu ya ustaarabu huu wa kisasa, sayansi na elimu.

122 Sasa hebu niwathibitishie ya kwamba elimu na ustaarabu vinatoka kwa Ibilisi. Sasa hebu na tugeuke hapa nyuma na tuone, kama mkitaka, katika Mwanzo, mlango wa 4. Vema, sasa hebu na tuanzie kwenye kifungu cha 16 cha Mwanzo 4. Kumi na nne hapa ama... Mwanzo 4, samahani. Sasa angalia, Shetani... .

123 Ninyi watu, mzifuate kanda hizi, pamoja na ndugu—ndugu yetu hapa, sasa, mmenisikia nikihubiri juu ya *Uzao wa Nyoka*, na hilo haliwezi kukanushwa. Huo ulifunuliwa katika moja ya hiyo Mihuri Saba. Ni jambo lilikuwa limefichwa.

124 Sasa kama watoto wamelelewa chini ya jambo la namna hiyo, unaona, chini ya mafundisho ya namna hiyo, hivyo ndivyo wazazi wao walivyokuwa, wana tabia ya wazazi wao, madhehebu yao, na kadhalika, inabidi waamini jambo hilo. Unaona, wanaamini jambo hilo kwa sababu wamezaliwa chini ya mzazi huyo. Lakini siku hizi hutuzaliwi chini ya mzazi yule; Mzazi wetu ni Neno. Nalo Neno... “Vema,” unasema, “Nilizaliwa chini ya Mungu, pia.” Kwa wakati huo. Lakini huu ndio wakati wa mwisho, huu ni wakati uliovuka madhehebu hayo.

¹²⁵ Ilibidi kuje, lazima kuje; Mungu alilikusudia kuwa hivyo, kwamba lazima kuje, hiyo Mihuri Saba sharti ifunguliwe. Jambo hilo lilipaswa kufanyika katika wakati huu wa Laodikia. Nami ninafikiri, bila tashwishi yoyote. . . Si kama vile tunavyojigamba; hatuna majivuno, ila tu juu ya Yesu Kristo; hakuna hata mmoja wetu. Tunajivunia tu juu ya Yesu Kristo. Lakini tunashukuru kwa ajili ya. . . kwa ajili ya majaliwa ya kujua kwa ninii yoyote. . . pasipo tashwishi yoyote, Mungu ametuchagua katika siku hizi za mwisho, na amethibitisha jambo hilo kwa ishara Mbinguni na duniani; na kila moja ya ishara hizo zikija moja kwa moja kurudi kwenye Neno, kuthibitisha ya kwamba ni kweli, wakati huu tunaishi, Ujumbe wenyewe na jinsi ulivyo. Sisi si madhehebu. Sisi si kundi la washupavu wa dini. Sisi ni watumishi wa Mungu, ambao wameitwa na Roho Mtakatifu. Mtabandikwa kila namna ya majina, bali hilo halimaanishi ndivyo ilivyo.

¹²⁶ Sasa kumbuka, mwana wa Shetani alikuwa ni Kaini. Sasa ninafikiri ninyi nyote mmepitia kanda zote, ambazo, ninaona maktaba zenu sehemu hizi, ya hizo. Sasa kumbuka ya kwamba Hawa alipewa mimba na Shetani, na siku hiyo hiyo. . . Tuna kisa cha jinsi hiyo huko Tucson sasa, ambapo mwanamke mmoja, kama akiwa. . . akiishi na wanaume wawili, anaweza akapata watoto wawili wa aina tofauti. Tunajua jambo hilo. Nililijua katika kuzalishwa kwa mbwa na kadhalika, na kadhalika, kama ni wakati uo huo.

¹²⁷ Kwa hiyo Shetani, asubuhi hiyo labda, alikutana na huyu mwovu, ambaye alikuwa ni nyoka; si reptilia, bali ni mnyama; mwenye hila sana, mjanja, mwerevu, kuliko hayawani wote, akiwa pungufu tu ya mwanadamu. Na mwanadamu ni mnyama, yeye mwenyewe, na sisi—sisi ni mamalia, wanyama wenye damu moto.

¹²⁸ Na—na Shetani alikuwa ndiye kiungo kinachofuata hapa, huyu nyoka, alikuwa ndiye aliyemfuata mtu, kutoka sokwe mtu, aliyesimama kati ya mwanadamu na—na sokwe mtu. Sasa sayansi inatafuta hicho kiungo kinachokosekana. Na kimefichwa kabisa hata ukimchanja vipandevipande, na hata hakuna mfupa ndani yake unaonekana kama wa mtu, unaona, ikimfanya awe reptilia.

¹²⁹ Sasa, tunaona sasa, ya kwamba, jamaa huyu alimkuta Hawa katika bustani ya Edeni, huyu kijana mwanamke asiyejua dhambi, ambaye hakujua uchi wake ulikuwa ni kitu gani. Naye nyoka alijua. Alikuwa mwerevu, mjanja, mwenye hekima. Ndipo nyoka akamwambia mwanamke, “Hiyo mbegu, ninii—hilo tunda lilikuwa ni tamu na lilikuwa linapendeza,” na. . . ndipo alipoishi naye asubuhi hiyo.

¹³⁰ Na basi, unaona, ndipo, alasiri hiyo, huyo mwanamke alimshawishi Adamu kufanya jambo lilo hilo, akimwambia kwamba tunda hilo lilikuwa ni nini.

¹³¹ Na ndipo Adamu kwa kudhamiria, akijua haikumpasa kufanya jambo hilo, alitoka akaenda na mkewe na kutenda tendo hili. Ambalo, hatimaye angelifikia hata hivyo. Lakini, unaona, ilibidi iwe hivyo, hekima ya Mungu, maana jambo hili basi, ambalo, linaonyesha sifa Yake kuwa Mwokozi, Baba, Mponyaji. Mmenisikia nikihubiri juu ya jambo hilo, mnaona. Sasa kama jambo hilo halikuwa limefanywa . . .

¹³² Yeye aliwaacha tu peke yao kule katika hiari ya kujichagulia wenyewe, kuwaacha wafanye wapendavyo. Asingeweza kuwafanya wafanye jambo hilo, na halafu awe angali ni mwenye haki. Bali angeweza kuwaweka wakiwa sawa na Yeye, na hiari ya kujichagulia, na halafu kuwaacha wafanye jambo hilo wenyewe. Naye alijua wangeweza kufanya jambo hilo.

¹³³ Na kwa hiyo basi, unaona, ndipo wakati Adamu alipoishi naye, alizaa mapacha. Na mmoja wao alikuwa ni wa Shetani; na mmoja wao alikuwa ni wa Adamu, ambaye alikuwa ni wa Mungu. Kaini na Habili.

¹³⁴ Na hilo hutukia. Tuna kisa kimoja kule Tucson sasa. Mwa—mwanamke mzungu aliishi na mumewe asubuhi moja, na alasiri hiyo akaishi na Mnegro. Na mmoja wa hao wavulana wadogo . . . Kulikuwa na wavulana wawili wadogo waliozaliwa. Mmoja wao alikuwa maskini Mnegro mwenye nywele za kipilipili, na huyo mtoto mwingine ana—ana nywele za shaba, mwenye sura nzuri sana. Na—na, wazia sasa, yeye huyo mwanamke anajaribu kumfanya huyo baba mzungu awatunze watoto wote wawili. Na mzungu akasema, “Nitamtunza wangu, bali si wake. Acha Mnegro amtunze mtoto wake mwenyewe.” Kwa hiyo, unaona, ni kweli.

¹³⁵ Daima kuna mapacha. Na hiyo ndiyo sababu . . . Msisahau jambo hili, enyi kundi dogo. Kanisa katika siku hizi za mwisho litakuwa na mapacha, “watafanana sana hivi kwamba itawapoteza hao walio Wateule . . .” Mathayo 24:24, unaona. Kanisa litaenda kuninii . . . Ni uamsho wa Kipentekoste. Unafanana sana na kitu kilicho halisi, hata “ingewapoteza walio Wateule kama yamkini.” Na baadaye kidogo, kama nikipata nafasi, ninataka kuelezea ni nini, jinsi uteule huo unavyokuja. Unaona, utawadanganya kwa kuwa ni karibu kama tu kitu kile kile. Unaona, baba wawili tu, hivyo tu; mama yule yule, kanisa lile lile, uamsho ule ule, kitu kile kile. Tuta ni lile lile, ambapo Neno linaangukia; bali mmoja wao, kama ilivyo hapa, amepotoka. Mnaelewa? Semeni “amina” kama kweli mnaliona. [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Unaona, mmoja wao ni upotovu, kwa sababu ni baba wengine. Jambo ambalo, nitawathibitishia siku moja, Mungu akiniruhusu, ya kwamba madhehebu ni alama ya mnyama. Unaona, ni baba wa uzinzi, yeye anawachochea watu kwenda kwenye madhehebu fulani badala ya kwenda kwenye Neno. Unaona, ni baba mwingine. Ni uamsho wa Kaini.

¹³⁶ Nitakapokwenda nyumbani wakati huu, ninahubiri juu ya somo, *Mkondo wa Nyoka*; yule mnyama hapo mwanzo, na yule mnyama hapo mwisho; na kumfuatilia moja kwa moja kote katika Biblia, na kuonyesha jinsi ambavyo anafikia kilele chake. Unaona? Na ninyi nyote mtapata hilo kwenye simu, mnaona, Bwana akituruhusu kufanya jambo hilo. Na sasa hebu angalia tu jinsi jamaa huyo alivyo mjanja, jinsi alivyo hasa ninii kabisa. . . Vema, wao ni kama tu Yuda na Yesu pale, wote wawili ni ndugu katika kabila lao, kama tu vile Esau na Yakobo. Na—na kama yule ku—kunguru na njiwa, waliokuwa wameketi kwenye kiota kile kile. Na kila kitu ni mapacha, katika—katika vita hivi vikuu tulivyo navyo.

¹³⁷ Adui hutumia uongo, kama vile alivyofanya kwa Hawa, “Loo, ati Mungu amesema? Hakika, lakini—lakini hakika. . .” Unaona?

¹³⁸ Unaona, kujaribu kulitilia hoja zaidi ya vile Mungu alivyosema hapo awali, “Mtakufa!”

¹³⁹ Yeye alisema, “Naam, Mungu alisema Hivyo, bali hakika. . .” Unaona hayo manyunyu juu yake? Unaona? Lakini yale Mungu asemayo, Mungu hutimiza, Yeye hahitaji msaada wowote kutoka kwa Shetani. Yeye hulitimiza. Kwa hiyo, kamwe msidanganywe na jambo hilo. Sasa tunaona, basi, ya kwamba hilo lilizaa kwa jinsi yake. Sasa katika Mwanzo hapa, tunaona, baada ya kunyunyiziwa kwa sumu hii ya maarifa.

¹⁴⁰ Sasa, sayansi ni maarifa. Na yote tunayosikia ni “sayansi, sayansi, sayansi, sayansi,” lile somo kuu shuleni, sayansi! Leo, gari zuri zaidi, *hili* bora zaidi, makazi bora zaidi, nyumba bora zaidi, *hiki* kizuri zaidi *kile* kizuri zaidi. Tunafanya kitu gani? Tunakufa, daima. Tuliumba gari, tukaacha kutembea; tukiacha kutembea, tutanenepa vibaya sana. Vema, hatuna mwanamume tena; tuna kiwavi. Hiyo ni kweli.

¹⁴¹ Na mwanamke, yote afanyayo, anatupa nguo, na halafu [Ndugu Branham anapigapiga kitu fulani—Mh.] anabonyeza kitufe, kwisha. Ambapo, mama yako alikuwa akitembea kwenda kwenye kijito, na kubeba maji, na kupasua kuni, na kuyachemsha kwenye birika mahali fulani, na—na kufua nguo zake namna hiyo. Na sisi ni wororo sana, kwamba kama wakifanya hivyo, ingetuaa. Lakini, hatuwezi kujisaidia, huu ndio wakati tunaishi.

¹⁴² Hata sayansi inasema sasa, ya kwamba, “Wasichana wadogo wanafikia kwenye ugumba, vijana wanawake kati ya umri wa miaka ishirini na ishirini na mitano.” Ninawakuta moja kwa moja kwenye mstari. “Kwamba vijana wanaume wanapitia katika umri wao wa makamu, kwenye umri wa kati ya miaka ishirini na ishirini na mitano.” Mama yangu. . . Mke wangu aliupitia, kati ya thelathini na mitano hadi arobaini. Mama yangu aliupitia, kutoka arobaini na mitano hadi hamsini.

Unaona jinsi wanavyozidi kudhoofika katika siku hizi za mwisho. Kwa sababu gani? Tunashughulika zaidi katika sayansi.

¹⁴³ Miaka mia moja na hamsini iliyopita, usafiri pekee ambao mwanadamu alikuwa nao ulikuwa ni wa farasi ama wa miguu. Na sasa anasafiri kwa jeti, karibu kama kwa wazo. Unaona, sayansi imefanya jambo hilo, na hilo ni la Ibilisi. Sasa unasema, “Hiyo ni kweli, Ndugu Branham?” Naam, bwana.

¹⁴⁴ Hebu na tuchukue Mwanzo sasa, 4.

Kaini akatoka mbele za uso wa BWANA, . . .

¹⁴⁵ Sasa angalia jambo la kwanza alilofanya. (Niambiieni mtakapooni tunayo ya kutosha hapa, maana nitasimama tu juu ya jambo hili mahali popote.) Unaona, “Kaini akatoka mbele za Uso wa Bwana.” Hapo ndipo alipofanya kosa lake. Na hapo ndipo utakapofanya kosa, na hapo ndipo nitakapofanya kosa, dakika ile ile tutakapotoka Mbele za Uso wa Mungu.

. . . Kaini akatoka . . . mbele za uso wa BWANA, akakaa katika nchi ya Nodi, mashariki ya Edeni.

¹⁴⁶ Unaona jinsi lilivyokuwa ni la kidini, akazunguka akaenda upande wa “Mashariki,” upande wa Mashariki.

Kaini akamjua mkewe; naye akapata mimba, akamzaa Henoko; naye Henoko akajenga mji, (unaona, ustaarabu), akajenga mji, akauita Henoko, kwa jina la mwanawe.

Na . . . Henoko akamzaa Iradi, Iradi aka- . . . Iradi aka- . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

. . . akajitwalia wake wawili; jina la wa kwanza ni Ada, na jina la wa pili lilikuwa Sila.

Ada akamzaa Yabali; na . . . ndiye baba yao wakaao katika hema na wanafuga wanyama.

Na jina la nduguye aliitwa Yubal; (nakisia, Y-u-b-a-l-i) huyo ndiye baba . . . wapigao vinubi na vinanda. (Unaona, muziki; sayansi, unaona, vikiingia.)

Sila naye . . . akamzaa Tubal-kaini, mfua kila chombo cha k-u-k-a-t-i-a, cha shaba na cha chuma; (kwa maneno mengine, kitu kama kufinyanga, kuunganisha pamoja), na umbu lake Tubal- . . . Tubal-kaini alikuwa Naama.

Lameki akawaambia wake zake, Sikieni sauti yangu, Ada na Sila; enyi wake za Lameki, sikilizeni usemi wangu; maana nimemwua mtu kwa kunitia jeraha; kijana kwa kunichubua.

Kama Kaini akilipiwa kisasi mara saba, hakika Lameki atalipiwa mara sabini . . . saba, ama mara saba.

¹⁴⁷ Sasa angalia, mara walipotoka mbele za Uso wa Bwana, walianza kujenga miji, walianza kutengeneza zana; wakaanza kuingia kwenye mambo ya sayansi, kufua shaba na chuma, na—na kupiga muziki, na kadhalika. Unaona? Unaona? Sasa hilo lilitoka wapi? Ni nani aliyetoka? Kaini, ule uzao wa nyoka. Mnalielewa? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Kaini alitoka. Na, angalia, yeye alitoka mbele za Uso wa Bwana, na akaanza kushughulika na mambo kwa sayansi.

¹⁴⁸ Sasa angalia mahali ambapo angali anashughulika, unaona: sayansi, elimu, miji, utamaduni. Ni vya Ibilisi. Ni nani aliyeviazisha? Ibilisi. Hayo ni ya akina nani leo? Ibilisi. Bomu za atomiki na zana mbalimbali, za kutuagamiza nazo. Tunaishi ndani yake. Inatubidi kuishi hapa. Sisi ni wanadamu, inatubidi kuishi hapa. Bali ule ustaarabu mkuu wa Mungu hautakuwa na chochote cha hayo ndani yake. Unaona? Na sayansi inachukua—inachukua vitu vya kawaida vya maumbile na kuvipotosha kutengeneza mambo ambayo hayakukusudiwa kufanywa.

¹⁴⁹ Na ndivyo ilivyo na dini ya kisayansi! Inachukua Neno la Mungu na kufanya shirika la kanisa kutokana nalo, badala ya kufanya mambo ambayo linapaswa kufanya.

Wanasema, “Siku za miujiza zimepita.”

Biblia ilisema, “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.”

“Hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu.”

¹⁵⁰ “Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio: Katika jina Langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya; wakishika nyoka, au kunywa vitu vya kufisha, havitawadhuru; wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.” Ati nini? Basi, mataifa yote, kila mtu, kila kiumbe! “Tazama, mimi niko pamoja nanyi, hata ukamilifu wa dahari, mwisho wa—wa mambo yote ya ulimwengu *kosmos*, jambo lote zima, mwisho wa ukamilisho.” Yeye yuko hapo kabisa!

¹⁵¹ Na sasa, unaona, wanachukua sayansi, na kusema, “Loo, vema, mradi tu tunakusanyika pamoja na kujiunga na kanisa, na tunakuwa *hivi*, ama mshiriki mzuri mwaminifu. Tunalipa ninii yetu. . .”

¹⁵² Unaona, si—si kule kusema, “Loo, hakuna kitu kama Mungu.” Mlisikia kanda yangu juu ya makristo wa uongo katika siku za mwisho. Unaona, si Yesu wa uongo (Shetani alijua vizuri zaidi, unaona), bali ni suala la makristo wa uongo. *Kristo* maana yake ni “aliyetiwa mafuta.” Na wao ni kweli wametiwa mafuta, wametiwa mafuta na (kitu gani?) Roho Mtakatifu, kufanya ishara na maajabu. Nao wanazifanya.

¹⁵³ Lakini, unaona, inapofikia sasa, tuko katika wakati wa mwisho, si huko nyuma katika wakati wa Upentekoste kule. Tuko huku katika wakati wa mwisho. Na wakati wa kwanza

ulianza na Neno, ambalo lilikuwa ni Kristo. Na wakati wa mwisho hauna budi kumalizikia na Neno, ambalo ni Kristo. Na mambo haya mengine, makapi haya na kadhalika, kama vile nilivyokwisha kuelezea, ni vibebaji tu vya Neno, kutimiza kusudi lake mpaka litakapofikia kimo kamili, unaona, wa vile punje ya asili ilivyokuwa.

154 Sasa kifungu cha 25.

Adamu akamjua mke wake tena; akazaa mwana mwanamume, akamwita jina lake Sethi; maana alisema, Mungu ameniwekea uzao mwingine mahali pa Habili; kwa sababu Kaini alimwua.

Sethi naye. . . Sethi naye akazaa mwana; akamwita jina lake Enoshi: Hapo ndipo watu walipoanza kuliitia Jina la BWANA.

155 Unaona jinsi ambavyo uzao huo wa nyoka ulivyoondoka ukaingia katika sayansi, elimu, miji, na muziki, na mambo makubwa, na elimu, na sayansi, na kadhalika.

156 Bali ule uzao wa mwenye haki, ambaye alikuwa. . . Unaona, Hawa hakuwa na mbegu. Mnajua jambo hilo. Mwanamke hana uzao, yule wa kike. Yeye ana yai, bali si mbegu. Lakini yeye mwanamke. . . alimwekea uzao wa kiume, uzao, unaona, aliwekewa na uteuzi wa Mungu, huyo mwanamke akabeba huo uzao. Nao yule Mzao mkuu, bila shaka, ambaye uliletwa na mwanamke, ndiye aliyetolewa na Mungu. Unaona, Mungu alimwekea uzao badala ya yule aliyeuawa na Kaini; ambapo, yule adui, mauti, uzao wa nyoka ulimwua mzao wa Mungu, katika upotovu pale, unaona. Mungu alimwekea, kupitia kwa mwanamke, Mzao, ambaye ni Kristo, unaona, ili kurudisha ule mzao wa asili tena. Unaona jambo hilo? Na kwa hiyo unaona huo upotovu ulileta mauti kupitia elimu na akili, na kile tunachoita siku hizi, sayansi na dini, na kadhalika, vilileta mauti. Lakini yeye mwanamke. . . alimwekea mwanamume, mzao, na ndipo watu wakaanza kuliitia Jina la Bwana, nao wakaanza kulirudia Neno tena. Unaona?

157 Basi kumbuka, fuatilia uzao huo, kwa kuwa tutaufuatilia katika majuma machache, juu ya huyu nyoka. Ukiufuatilia huo, unapitia moja kwa moja katika Maandiko. Uangalie. Hiyo mizabibu miwili inakua moja kwa moja pamoja, kama vile mlivyosikia ujumbe wangu juu ya “ule mzabibu.” Ilikuwa moja kwa moja pamoja, na inafanana sana hata karibu ingewapoteza wateule wa kweli, kama yamkini, katika siku za mwisho wakati inapofikia kilele chake. Inazaa punje kama ngano tu, bali si ngano, unaona, siyo. Ni kapi, bado.

158 Sasa, angalia pale: ustaarabu, elimu. . . Nafikiri nina kama Maandiko mengine kumi, mnaona, yaliyoandikwa hapo chini, lakini nafikiri nisyapitie hayo. Lakini tunafahamu kwa jambo hili, ya kwamba elimu, sayansi na ustaarabu, ni vya Ibilisi. Hiyo

ni kweli. Si vya Mungu. Ni vya Ibilisi. Sasa, sisemi haikupasi kuwa navyo. La, sivyo kabisa. Baadaye kidogo, ninaweza, tutathibitisha jambo hilo; ya kwamba Mungu. . .

¹⁵⁹ Ni kama vile tu ninyi mkivaa nguo, ninyi wanawake, sisi wanaume. Hatukupaswa kuvaa nguo, hapo mwanzo. Lakini, unaona, kwa kuwa tunaishi katika wakati huu tunaishi, hatuna budi kuvaa nguo, unaona. Tumeamriwa kufanya hivyo. Hatuna budi kuzivaa. Lakini hapo mwanzo, haikulazimu tuvae nguo, unaona, kwa kuwa hatukujua dhambi yoyote. Lakini sasa tunapaswa kuzivaa.

¹⁶⁰ Sasa inatubidi kuwa na magari. Sasa tunapaswa kwenda mahali mbalimbali na kuzuru, na kadhalika, katika magari na sayansi, na kadhalika, bali si vya Mungu. Si vya Mungu. Elimu mbalimbali, bali vinaninii. . .

¹⁶¹ Muundo wa elimu ya Mungu, ustaarabu, sayansi, viko katika hali yake ya asili, unaona, vimepita mambo haya tunayofanya.

¹⁶² Sasa angalia, wanachukua vitu fulani na kuchanganya vitu fulani pamoja, na vinatengeneza kemikali ambayo itaangamiza. Sasa viache vitu hivyo katika hali yao ya asili, havina shida; ukivichanganya, vyote vinakuwa ni vibaya. Unaona? Unaona, inaleta mauti.

¹⁶³ Na unapojaribu kulichukua Neno la Mungu na kuliweka katika dini ya ulimwengu huu, unajiletea mauti mwenyewe. Inamwua mtu huyo. Unaona kile ninachomaanisha? Inamwua mtu huyo. Unasema, “Vema, sasa angalia, unamwamini Mungu.” “Loo, sasa, haikulazimu kuamini jambo *hilo*. Kama we—we—we . . . kanisa letu.” Papo hapo, huo ndio mlipuko unaomwua—inayomwua mtu.

¹⁶⁴ Inakubidi kuachilia kila kitu kiondoke, na kuchukua Neno pekee yake. Dumu moja kwa moja na hilo Neno. Usiliache. Wakati Mungu aliposema hivyo, hivyo ndivyo tu ilivyo. Sijali yale elimu inayoweza kuthibitisha.

¹⁶⁵ Katika siku za Nuhu, waliweza kuthibitisha hakukuwa na maji huko juu angani. Lakini Mungu alisema maji yalikuwa yakija, nayo yakaja. Hiyo ni kweli.

¹⁶⁶ Wao wanasema leo, “Hakuna moto huko juu, wa kuanguka.” Bali uangalie huo ukianguka, siku moja. A-ha. “Tufanyeje jambo *hili* na kufanya jambo *lile*?” Mwangalie Mungu akilifanya. Yeye atalifanya. Alisema litafanyika.

¹⁶⁷ Na Mbegu hiyo itashika mahali fulani. Utukufu kwa Mungu! Jambo pekee analotafuta, leo, ni tuta, mahali fulani inapoweza kuota.

¹⁶⁸ Itaanza katika mtu fulani, nao wataipotosha, na kuinyunyizia kama alivyomfanyia Hawa. Lilianza katika Hawa, kwa yeye kubeba mbegu na kuzaa wana wa Mungu, si wana wa Shetani. Lakini yeye alikuwa ni tuta la kuzalishia,

nayo iliangukia mahali pabaya. Vivyo hivyo Neno litaangukia katika mtu asiyeamini, ama mwenye kushuku, ama asiyesadiki. Litamfanya mfuasi wa kanisa, bali si mwana wala binti ya Mungu kamwe. Wewe waambie kuziacha nywele zao zikue; watakucheka waziwazi. Ukiwaambia wafanye *hivi* ama *vile*, ama mwanamume afanye jambo fulani, watakucheka waziwazi. Si wana wa Mungu. Ni tuta baya la kusia, hata hivyo wanashikilia ile Mbegu. Unaona waliopakwa mafuta wa uongo? Wamepakwa mafuta, naam, kwa Roho Mtakatifu, wananena kwa lugha, na kufanya ishara na maajabu; bali ni ya Shetani.

¹⁶⁹ Yesu alisema, “Wengi watakuja Kwangu siku hiyo, na kusema, ‘Bwana, Bwana, sikutoa pepo, na—na kufanya kazi kubwa na za nguvu na maajabu katika Jina Lako?’” Yeye alisema, “Ondokeni Kwangu, ninyi mtendao maovu.”

¹⁷⁰ Uovu ni nini? Daudi alisema, “Kama ningaliwaza maovu moyoni mwangu, Mungu hatanisikia.” Unaona?

¹⁷¹ Uovu ni jambo unalojua kwamba unapaswa kulifanya wala hutalifanya. Unajua vyema zaidi, bali hutalifanya. Ni uovu, unaona. Unajua wanapaswa kudumu na Neno la Mungu, bali kwa ajili ya kanisa, ama kwa ajili ya mtu mwingine, ama kitu kingine, utaliacha Neno la Mungu na kufanya yale madhehebu yanayosema. “Vema, sijui. Kanisa langu linasema tunapaswa kufanya jambo hilo *hivi*, nami ninaliamini *hivi*.”

¹⁷² Unaona, nalo lipo moja kwa moja mbele zako ya kwamba hupaswi kulifanya jambo hilo. Huo ni uovu. “Ondokeni kwangu, ninyi mtendao uovu.”

¹⁷³ Mwangelie yule Mtakatifu maarufu Paulo, katika I Wakorintho 13, yeye alisema, “Nijaposema kwa lugha ya wanadamu na ya Malaika...” Sasa ninyi mnaotaka, ama mtu fulani anayetaka, kushikilia hilo je, hilo ndilo thibitisho la Roho Mtakatifu? Paulo alisema, “Nijaposema kwa lugha kama wanadamu na Malaika, wala sina upendo” kama mlilo nao ninyi nyote hapa miongoni mwenu, “Si kitu mimi.” Unaona?

¹⁷⁴ Unaweza kunena kwa lugha, naam, kwa kuwa ni Neno. Mhubiri anaweza kuchukua Neno hili, na kwenda na kulihubiri, na kuhubiri Neno hilo, na Neno hilo litakua. Lakini mhuhubiri huyo angeweza akawa ni mnafiki, yeye mwenyewe. Ni Neno. Unaona? Lakini kiumbe cha kweli kilicho hai cha Mungu huchukua kusudi lote, Neno. “Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu.” Nawe unaongeza kitu kingine kwa Hilo, una mmea uliopotoshwa.

¹⁷⁵ Kama nikianza hapa nje na ngano, na niweke gu—gugu pamoja nayo, na kuzizalisha pamoja, kama ingeweza kufanywa hivyo kwa chavua, na kuwekwa mle ndani, nina gugu-ngano. Unaona? Linaonekana kama ngano, na hata hivyo ni gugu. Si uhai halisi, haliwezi kujizaa tena. Unaona? Litaota, bali haliwezi kujizaa la aina yake tena.

176 Pu—pu—punda anaweza kuzaa na farasi jike, naye atamzaa nyumbu, bali nyumbu huyo hawezi kumzaa nyumbu tena. Ni chotara.

177 “Kila neno na lizae kwa jinsi yake.” Unaona, anaweza kuzaa mara moja. Nalo kanisa linaweza kuja kama madhehebu, mara moja, bali haliwezi kujizaa tena; linaleta madhehebu mengine. La Kilutheri haliwezi kuzaa la Kilutheri; lilizaa la Kimethodisti. Nalo la Kimethodist likazaa la Kipentekoste. Unaona, haliwezi kujizaa lenyewe tena, kwa kuwa limekufa. Haliwezi kuanzisha ufufuo. Ni wapi ambapo Mungu aliwahi kuanzisha ufufuo katika madhehebu? Angalia kwenye historia yako. Hajawahi. Madhehebu ndiyo yanayoundwa kufuatia ufufuo.

178 Wakati Luther, yule mtu wa Mungu, alipojitokeza na ujumbe wa kuhesabiwa haki, nyuma yake lilikuja kanisa la Kilutheri. Wasingeweza kamwe kuweza kukua.

179 Ndipo Mungu akamtuma mtu kwa jina la John Wesley, kukatokea ufufuo nyuma ya huo. Nao wangepanya nini? Wakauundia madhehebu. Lisingeweza kamwe kujizaa tena. Unaona, ni tasa.

180 Haleluya! Bali Neno la Mungu litadumu milele! Hiyo ni kweli. Litazaa kwa jinsi Yake.

181 Huu hapa wa Kipentekoste unakuja, yeye hawezi; angalia kile ulichofanya, uliunda madhehebu. Haliwezi kujizaa tena. Wanaweza kuwa na akina Oral Roberts na chochote kile, kote nchini, haliwezi kujizaa tena. Litaendelea kushikilia moja kwa moja kwenye mambo ya huko nyuma ya uzao huo wa kawaida wa nyumbu. Haliwezi! Haidhuru liingiziwe akina nani wangapi, linabaki vile vile lilivyo; hata liwe lina mambo mangapi ya kiroho, na kitu chochote lilicho nacho, ni ninii... Ninyi, sasa ninyi ni watu wazima, mnajua ninachonena habari zake. Haidhuru lina waume wangapi na wake wangapi, na chochote kile, na hata liwe na makanisa-shirika mangapi linaloanzisha huku nje, na makanisa madogomadogo na mashirika, haliwezi kuleta ufufuo. Limekwisha. Limechanganyikana na ulimwengu, kutoka kwenye Neno la Mungu, wala haliwezi kujizaa tena. Mungu atainua kitu fulani kingine na kuanza kulifanya Neno Lake liendelea mbele; na kama likiunda madhehebu, litakufa pia! Hiyo ni kweli. Haliwezi kujizaa lenyewe tena, kwa kuwa ni chotara. Hiyo ni kweli.

182 Angalia mahindi yako ya haibridi leo, eti wanasema, “Ndiyo mahindi yaliyo mazuri kuliko yote.” Ni kitu—ni kitu kinachoua. Ndiyo yanayowaua. Uhai wenu haukufanywa kwa ajili ya... Miili yenu haikuumbwa kutumia kitu hicho. Miili yenu iliumbwa kutumia punje ya asili. Hiyo ndiyo sababu baba zenu na mama zenu, na wengineo, waliishi muda mrefu zaidi. Hiyo ndiyo sababu walikuwa ni wenye nguvu. Mtu, mwenye umri wa miaka sabini na themanini, alikuwa shupavu na mwenye

nguvu. Unaona, waliishi kwa kula vitu vya asili. Waangalie hawa wanaume wazee wanaoishi milimani kwenye sehemu hizi, wanaishi kwa nyama ya ayala na—na nafaka za asili. Mweke mtu hapa, mjini; huyu hapa anakuja, ni mtu mnene sana, kwenye umri wa miaka kama thelathini na tano, arobaini hivi. Ni mwororo? Bila shaka! Vema, ninaliacha somo langu, sivyo?

¹⁸³ Angalia, bali ninajaribu kuwaambia jambo fulani, nalo ni ustaarabu, kile tunachoita utamaduni. Utamaduni, watu mnasikia mengi sana juu ya kitu hicho. Sasa, Je! mlipata kusikia makisio yangu ya utamaduni yalikuwa ni nini? Ni mtu asiye na ujasiri wa kutosha kumwua sungura, bali anaweza kula nyama yake kiasi cha kumtosha baada ya mtu mwingine kumwua. Kwa hiyo, mimi, hivyo ndivyo ni—ni—ni—ninavyofikiria juu ya utamaduni, mnaona. Hiyo, hiyo ni kweli, mnaona. Hatuninii . . .

¹⁸⁴ Mungu haji kwa . . . Si kumwingiza mtu kwa Mungu kwa *utamaduni*. Humwingizi kwa Mungu kwa *kumstarabisha*. Yeye anazaliwa, mbegu ya Mungu, kutoka kwa Mungu, daima ilikuwa ni Mungu, wala haiwezi kuwa kitu kingine chochote kamwe ila Mungu. Huingizwi Kwake kwa utamaduni.

¹⁸⁵ Sasa, jinsi alivyo na Edeni ya aina yake, na kwa mbegu iliyumbuliwa! Shetani ametengeneza yake maarufu naye pia, Edeni yake maarufu sasa. Ni ya namna gani? Utamaduni, sayansi, makanisa mazuri, minara mirefu, wahubiri wazuri walioadibika, elimu: “DA., D., Ph.D., LL.D., Dakitari wa Fasihi, Dakitari wa Thiolojia, Madaktari!” Kila unapotamka kitu hicho, kinampeleka tu kiasi hicho mbali zaidi na Mungu, kinamtupilia tu mbali moja kwa moja. Na kusanyiko halitaki mtu fulani kusimama pale na kutumia maneno ya “iki, akiko, na ote, na pepa na tukua.” Hawataki hayo. Wanataka kitu fulani cha kupendeza.

¹⁸⁶ Ndicho kitu kile kile ambacho Kaini alikuwa nacho niani mwake, (baba yao, hapo mwanzo), alitoa sadaka maua na matunda ya shambani. Wakati, Mungu alitaka dhabihu, mtu mwenye ufunuo wa Mungu! Ilikuwa ni damu! Si pea, wala pichi, wala plamu, ama chochote kile, ama aprikoti, kama wanavyosema siku hizi. Damu ndiyo iliyotutoa kutoka katika bustani ya Edeni, da—damu iliyoharibika, mwanamke aliyeruhusu mbegu ya mtu mwingine ipandwe katika tumbo la uzazi na kuanzisha matatizo.

¹⁸⁷ Sasa tunaona, ili kuthibitisha ya kwamba Ujumbe uko katika wakati mwafaka kabisa, yale ninayowazungumzia, ili kulithibitisha hilo, angalia katika siku za kuihaibridi leo hii, wakijaribu kufanya spishi ya kupendeza zaidi. Angalia katika kuhaibridi. Angalia uhai wa mimea. Hapa kwenye msimu wa kiangazi uliopita . . .

¹⁸⁸ Ilikuwa kwenye msimu huu wa kiangazi, ilikuwa msimu wa kiangazi, nilikuwa na ua dogo la mwituni (alilokuwa

akinionyesha huko nje dakika chache zilizopita, nimekumbuka jambo hilo), ua dogo moja la mwituni nililokuwa nalo hapa kwenye tuta, ilibidi niliangalie hilo mara mbili kwa siku, kulifanya liishi. Lilikuwa ni haibridi. Lakini lilitokana na ua lingine dogo la manjano, ambalo lilizalishwa pamoja na kitu kingine, kufanya ua hili.

¹⁸⁹ Na jamaa huyo mdogo alisimama huko nje, wakati, ungeweza kuchimba futi kumi ardhini wala usingepata hata unyevu wa kutosha wa kunyunyizia. Unaona, lilikuwa—lilikuwa—lilikuwa tu likiishi mavumbini, na lilikuwa zuri tu vile vile, wala halikuhitaji kunyweshewa maji. Lilikuwa ni la asili. Halikuwa ni haibridi. Hakukuwa na kitu kilichochanganywa nalo, lilikuwa ni ua halisi.

¹⁹⁰ Na hili lilikuwa limechanganywa na kitu fulani, inakubidi kulitilia maji na kulibembezeza, na kulidekeza. Unaona? *Hili* haikubidi ulifanyie hivyo; hakuna wadudu waliolishambulia. Inatulazimu kulipiga dawa, na chochote kile, kuwafukuza; na nzi na usubi na kadhalika, kuwafukuza namna hiyo. Usipofanya hivyo, wangeyaua.

Huhitaji, usubi usingelika ribia!

¹⁹¹ Loo, huyo ni Mkristo halisi, wa kweli, aliyezaliwa mara ya pili. Ungeweza kumjaribu na chochote unachotaka. Yeye angali ni Mkristo. Mjaribu popote unapotaka kuwa, yeye angali ni Mkristo.

¹⁹² Maskini bibi mdogo kutoka katika mmoja wa ndugu hapa, baadhi ya watu wenu, kanisa lao aliniandikia barua hivi majuzi. Kasema, “Baba hataki niende kwenye besiboli... ama mchezo wa mpira wa kikapu, Ndugu Branham. Tunaamini...” Akasema, alikuwa na umri wa miaka kumi na miwili, kasema, “Ndugu Branham, tunaamini wewe una Neno la Bwana, katika lolote unalotwambia sasa.” Kasema, “Kwa namna fulani ninafikiri baba yangu anakosea. Lakini,” kasema, “lo lote utakalosema, nitaliamini.” Sasa, maskini msichana huyo mpenzi, unaona.

¹⁹³ Kwa hiyo nikawazia. “Vema,” nikasema, “kipenzi, angalia kama wewe ni Mkristo, wewe ni Mkristo mahali popote. Haidhuru uko wapi, ungali ni Mkristo. Lakini,” nikasema, “unaona, kwenye uwanja wa mpira wa kikapu, yale baba anayowazia, unawasikia hao watoto wakilaani na kufanya makelele namna hiyo. Ningali ninaamini ungekuwa ni Mkristo. Lakini, unaona, Baba amesonga mbele zaidi katika maisha kuliko wewe. Unaona?” Sasa, nikasema, “Sasa wewe una umri wa miaka kumi na miwili, na ulisema ulikuwa na dada mdogo, minne. Sasa yeye anataka utengeneze wanaserere wa karatasi. ‘Loo, endelea, sina wakati wa kutengeneza wanaserere wa karatasi.’ Unaona, wewe una umri mkubwa kuliko huyo dada mdogo.”

¹⁹⁴ Sasa, hapo ndipo kanisa linapopaswa kuwa siku hizi, kukomaa zaidi katika Neno la Mungu. Si Methodisti, Baptisti, Wapentekoste, Mpresbiteri; bali kukomaa katika Neno, kuwa wana na binti za Mungu. A-ha! Vema. Vema. Ujumbe ukiwa katika wakati unaofaa, umethibitishwa.

¹⁹⁵ Kwa sayansi, kwa sayansi yake na utafiti, unaona, wao wamejaribu kupotosha kila kitu, kufanya mbegu ya aina ya tofauti, kufanya kitu fulani cha tofauti, kukifanya cha kupendeza zaidi.

¹⁹⁶ Angalia dada zetu. Nilitoa tamshi muda mfupi uliopita, kuhusu jinsi walivyoonekana wanapendeza. Loo, unaweza kuwasimamisha hapa nje katika mashindano ya dunia pamoja na baadhi ya hii ya Gloria Swanson, ama baadhi ya hawa wavua nguo na kadhalika huku California, nao wengeweza kushindwa kwa maili milioni kadhaa. Bali majina yao hayamo kwenye kile kitabu cha sifa; yamo kwenye Kitabu cha Uzima, unaona. A-ha. "Roho ya upole na utulivu ni ya thamani kuu kwa Mungu." Na Biblia ilisema wa—wanawake wetu "wajipambe kwa roho ya upole na utulivu, mkiwatii waume zenu, na utu wema." Hicho ndicho chenye thamani kuu mbele za Mungu. Unaona? Hiyo ni kweli.

¹⁹⁷ Si hawa wote walio hapa, hivyo ndivyo walivyofanya; wao, Max Factor, imewarembesha wanawake, kwa nje, jambo ambalo ni la Shetani. Upuuzi huo wote ni wa Ibilisi. Je! ulijua jambo hilo? Hakika. Upuuzi huo wote ni wa Ibilisi.

¹⁹⁸ Sasa ninakumbuka maskini mke wangu wakati alipokuwa anapendeza na ni kijana, hakujipodaa. La. Alikuwa, nikambatiza katika Jina la Yesu, wakati alipokuwa amevaa nguo fupi iliyofikia magotini namna *hiyo*, unaona. Lakini sasa anazeeka, alisema, "Ninaingiwa na makunyanzi sana."

¹⁹⁹ Nikasema, "Unajua, jinsi unavyokuwa mzee, ndivyo macho yangu yanavyozidi kufifia. Ninakukumbuka jinsi ulivyokuwa, nami ninakumbuka na ninajua moyoni mwangu jinsi utakavyokuwa siku moja. Unaona? Unaona? Unaona, ukiwa na roho ya utulivu na ya upendo uliyo nayo, Mungu atatuweka pamoja tena huko ng'ambo. Hivyo ndivyo ilivyo, ndipo hatutabadilika tena basi." Kwa hiyo kwa nini . . .

²⁰⁰ Lakini, unaona, katika siku za Nuhu, wakati wana wa Mungu walipowaona binti za wanadamu, walikuwa wazuri sana, walijitwalia wanawake, wawe wake zao. Mnaona, wana wa Mungu waliwaona binti za binadamu, maana walikuwa wakware na—na walivaa kiasherati. Wao, waliwatamani wanawake hao, nao wakaenda kuwachukua, mnaona.

²⁰¹ Nina furaha ya kwamba ninyi wana wa Mungu mnaona mbele zaidi ya jambo hilo, unaona, jinsi ambavyo wanawake wanavyojiweka. Unaona?

²⁰² Lakini ni kitu gani? Kila kitu ni urembo. Ni uchotara. Chukua baadhi yao, waoshe uso wao, wao...usingejua kile ungekuwa nacho. Unaona? Na hiyo ni kweli. Labda hasira ya kutosha kupigana na msumeno uvumao, na—na ni wafisadi, na—na wakaidi, na wachafu, na wanatembea na mwanamume mwingine.

²⁰³ Sijali nini, mke wangu, ni—ninaheshimu uaminifu katika mwanamke yeyote. Nilipokuwa mvulana mdogo, daima nilisema, “Kama mwanamke wa kinegro alitaka kuwa mwaminifu, ningemwaga tone la mwisho la damu yangu kumweka jinsi hiyo.” Unaona, ninaheshimu mambo yaliyo mema, jambo jema. Nimejaribu kuishi hivyo, maishani mwangu mwote. Nilikuwa kijana wakati huo, sasa mimi ni mzee, sijabadilisha mawazo yangu hata kidgo. Unaona?

²⁰⁴ Sayansi, kwa picha ile ile Hawa alivyofanya, yeye pia amefanya jambo hilo kwa kanisa, kulipotosha. Alitekeleza mipango yake siku hizi, kupitia katika kanisa lake chotara, Edeni yake ya kisasa tuliyo nayo leo. Tunaishi katika Edeni ya kisayansi, Edeni ya Shetani, Edeni ya kisayansi.

²⁰⁵ Kama mngetaka kuifungua, katika Isaya 14:12. Nitawanukulia, kama mkitaka, kama mkitaka, 12 na 14..

...Shetani akasema moyoni mwake, *nitapaa kupita vimo* vya Yeye aliye Juu.

Angekuwa na ufalme, hata ingekuwa kwamba wana wa Mungu wangelimwabudu.

²⁰⁶ Na hivyo ndivyo hasa amefanya. Amefanya jambo hilo kupitia kwenye kanisa, dini, kama alivyoanza hapo mwanzo, dini. Amefanya jambo hilo.

²⁰⁷ Pia kama vile nabii Paulo alivyoona, katika II Wathesalonike mlango wa 2, ya kwamba yeye—yeye anaelekea katika E... ninii yake, hiyo Edeni kuu ya kisayansi katika siku hii, katika kisayansi, katika elimu na ustaarabu. Naye amejitengenezea, yeye mwenyewe, na hatimaye ataishia kwenye halmashauri ya ekumeni, mahali ambamo makanisa yote yatalazimika kumwabudu. Basi mnaona ni kitu gani? Ni yule roho wa udanganyifu akitenda kazi miongoni mwa watu; wana wa Mungu, ambao wamefanywa katika sura ya Mungu; na binti za binadamu, ambao wamefanywa katika sura ya binadamu; amewachukua chini ya udanganyifu, kama alivyomfanyia Hawa. Na amejiundia, mwenyewe, kwa vitimbi vyake mwenyewe vya sayansi na elimu na utamaduni, mpaka amejipatia Edeni ya kisasa, ya kisayansi, ya mauti.

²⁰⁸ Ambapo, Mungu, kwa Neno Lake, alinena, Naye akakuwa na Edeni isiyo na mauti; isiyo na sayansi, isiyo na elimu kama tuliyo nayo leo, ama bila ustaarabu.

209 Je! unaona jambo hilo sasa, unalielewa? Unaona, sasa yeye ana Edeni yake. Angalia, makanisa yote yanamwabudu. Hivyo ndivyo...katika Wathesalonike wa Pili hapa, Yeye alivyosema.

...mtu huyo anayejiita Mungu, ameketi *katika hekalu la Mungu*,...

Na wote...juu ya nchi watasalimu amri na watamsujudu, kila ambaye jina lake halikuandikwa katika kitabu cha uzima cha Mwana-Kondoo...kabla ya kuwekwa misingi dunia.

210 Unaona, ni Edeni ya kisasa. Sasa yeye anafanya nini, yeye mwenyewe? Anajisogeza, Rumi, mahali pake pakuu pa mwisho pa kula, Edeni.

211 Mnaona hapo mahali ambapo huyo papa alipokuja huku hivi majuzi? Mlizonia zile kumi na tatu zote zilizotukia wakati huo? Alizungumza maneno kumi na matatu, akawapa watu kumi na watatu ushirika, akazungumza kwenye Uwanja wa Michezo wa Yankee, ambao ni kumi na tatu. Kila kitu kilikuwa ni kumi na tatu.

212 Na nambari ya taifa letu ni kumi na tatu, linaonekana katika mlango wa 13 wa Ufunuo; milia kumi na mitatu, nyota kumi na tatu, milia kumi na tatu, namba kumi na tatu kwenye sarafu, nyota kumi na tatu kwenye sarafu, kila kitu ni kumi na tatu, na ni mwanamke.

213 Huyu hapa papa anakuja, kiongozi, kwa mwanamke huyo; mpinga Kristo wa uongo kwa bibi-arusi wa uongo, wa sayansi. Ambapo, ulimwengu wetu, ulimwengu wetu wa mashariki hapa wa Kimarekani hapa, ama Ulimwengu wa Kimagharibi, umeuongoza ulimwengu, katika sayansi. Anakuja kwake, katika kanisa lake la kisayansi, na sasa Waprotestanti wote wanamsujudia, unaona, kwenye kumi na tatu. Unaona jambo hilo? Kila kitu kiko katika kumi na tatu. Taifa letu lote, kila kitu kinginecho, ni kumi na tatu, ulimwengu wa mwanamke. Unaona, tumewasili, tumepata kulijua. Ulibadilika kuwa ulimwengu wa wanawake katika bustani ya Edeni, bali utakuwa ni ulimwengu wa Mungu siku moja. Angalia sasa.

Sasa, pia, manabii hawa na kadhalika wametabiri jambo hilo.

214 Na sasa yote tena yamekuja kama ilivyokuwa kabla Mungu hajasogea juu ya nchi, imekuwa ni machafuko ya kiroho. Bila shaka, yamekuwa hivyo ni machafuko ya kiroho.

215 Hapa angalia Edeni ya pili imefananishwa vizuri sana na ile ya kwanza, kudanganya, karibu kuwachukua walio Wateule. Angalia sasa, jambo hilo. Nitalinganisha hapa, kwa dakika chache tu. Sasa itanibidi kukoma, maana ni saa tano, na kwa hiyo sikilizeni. Edeni hizi mbili, jinsi ambavyo Edeni hii imejaribu kuwa mfano, kama tu vile Shetani alivyofanya pale

mwanzo, kwa Hawa katika Edeni halisi, ile Edeni ya kwanza. Zianganalie tu, zimefananisha pamoja sasa. Unaona, tumelipata, sasa kila mtu anafahamu dhahiri, Edeni ya kisayansi tunayoishi. Unaona? Sasa, haikuwa ni Edeni ya Mungu.

²¹⁶ Edeni ya Mungu haiji kwa sayansi, elimu, utamaduni. Inakuja kwa Neno, unaona, ikiita vitu hivi vyote kana kwamba havikuwa. Na tazama, katika bustani ya Edeni...Hebu na tuzilinganishe tu kidogo. Sasa angalia.

²¹⁷ Yule mtu na mke wake, (mkuu, katika... bustani ya Edeni), hao wawili walikuwa uchi wala hawakujua hilo. Hiyo ni kweli? Katika Edeni ya Mungu, hao wawili walikuwa uchi wala hawakujua jambo hilo.

²¹⁸ Sasa hao wako uchi tena wala hawajui, Ufunuo 3, Wakati wa Kanisa la Laodikia.

Kwa kuwa wewe...ni uchi, mwenye mashaka, maskini, mnyonge, kipofu, wala hujui.

²¹⁹ Sasa, katika Edeni ya Mungu, walikuwa uchi wala hawakujua. Na sasa katika Edeni ya Shetani, ikiwa ni kwa sayansi na elimu, wao ni uchi tena wala hawajui. Ni upotovu jinsi gani!

²²⁰ Angalia leo. Mwangalie mwanamume, akijiingiza kwenye kuvaa nguo za mkewe za ndani; naye mke ajiingiza kwenye kuvaa nguo za mumewe. Na mwanamume anachachamaa kuachilia nywele zake zikue kama za mwanamke; naye mwanamke anakata zake kama za mwanamume. Loo, loo, loo, jamani! Wanaume wakichacha kuwa wanawake, wanawake wakishupaa kuwa wanaume, upotovu!

²²¹ Hilo ndilo jambo lile lile kanisa linalofanya, jambo lile lile, Wakati wa Laodikia. Angalia.

²²² Sababu ya wao kutojua walikuwa uchi, hapo mwanzo, kulikuwa na utaji wa Roho Mtakatifu ukiwafunika wasiwe uchi. Hawakujua jambo hilo. Roho Mtakatifu alikuwa kwenye macho yao, hawakuona kitu ila ndugu yao na dada yao, unaona. Hizo sheria, hawakujua walikuwa uchi. Roho Mtakatifu!

²²³ Sasa roho wa uchafu, zinaa na tamaa mbaya, amewatia utaji; elimu, sayansi, "Mbona, ni la kisayansi. Vaa kaptura, husikii joto." Wahindi wanawafundisha vizuri zaidi kuliko hivyo. Wao wanajifunika blanketi, wapate kuyoyozwa, unaona, na kuvaa nguo. Unaona, elimu imerudi nyuma kabisa kufikia wakati, jambo lile lile wanalifikiria kwamba limewaleta kwenye utamaduni na ustaarabu, limewarudisha kwenye ujinga tena, wakawa wabaya zaidi kuliko walivyokuwa hapo mwanzo.

²²⁴ Masomo, elimu, aangalia hizo shule! Angalia kule katika chuo kikuu, hivi majuzi usiku, hao wavulana! Ni watoto wangapi wanaozaliwa na hao mabibi vijana kule, kwa hao mabibi wadogo kila mwaka kwenye chuo kikuu! Hebu wazia! Unasema, "Huu

ni upuzi wa mitaani.” Na hao wavulana, hao “lulu wa ishirini na moja,” wanavyowaita, wakiwa wamejipaka rangi mdomoni, na—na nywele zimechegwa usoni, na kusokotwa katika misokoto na kuning’inia chini. Wanasema hivyo. Na wenye busu za ngono, wachafu! Unasema, “Vema, hizo ni takataka za mitaani.” Ati nini? Ni wanafunzi wa chuo kikuu.

²²⁵ Walilewa sana, hivi majuzi usiku. Wala hawakujua la kufanya, na kwa hiyo, walitaka kujifurahisha. Na kunywa pombe na uzinzi, na kila kitu namna hiyo, havikuwatosha. Walivunja chupa, na kukimbia kwenda mpaka kwenye mlango wa wanawake, na kubisha mlango; wakatoka, wakawapiga makofi usoni. Wakakatilia mbali jicho la msichana mmoja, na wengi sana wakaumbuliwa kabisa maisha. Unafikiri wangetangaza jambo hilo? La.

²²⁶ Wawili wa wavulana wao wakiendesha gari huku na huko mtaani, na wanawake wawili vijana walioolewa wameketi kwenye—kwenye vipandio, nao wakawabaka wanawake hao. Polisi waliwakamata wakawaweka gereza. Mshauri wa wanachuo alishuka akaja kule. Na kitu hicho chote kinastawi kwenye chuo hicho kikuu, hizo ndizo kazi tu walizo nazo huko. Kasema, “Hao ni watoto wangu. Waachilieni.” Wakawaachilia.

²²⁷ Mambo ndiyo hayo; ustaarabu, elimu, vinaelekeza kwenye mauti na machafuko, na kuzimu. Msisikilize upuuzi huo. Angalia sasa.

²²⁸ Hawa ilimbidi kuchungulia kidogo tu, apate kuona vile ulimwengu ulivyoonekana. Unajua, mara nyingi, “Inatubidi kuvaa tu sehemu ndogo ya *hiki*.” Ama, unajua ninalomaanisha, inakubidi tu kuchungulia kidogo tu, upate kuona. Sasa katika Yohana Mt. ama...

²²⁹ Yohana wa Kwanza 2:15, Mungu alisema, “Ukiipenda dunia au hata kuwa na upendo wa dunia, kumpenda Mungu hata hakumo ndani yako.” Mambo yaliyo huko nje yamekufa. Umetahiriwa, ukakatiliwa mbali nayo. Hutaki mambo ya dunia, umefafia. Yamekufa. Wewe hutaki chochote kilichokufa. Kimeoza. Kinanuka. Kitu fulani kilicho hai kitamani vipi kitu kilicho kichafu kama hicho? Unaona, wewe u hai katika Kristo. Neno linakufanya hai.

²³⁰ Jamani, ninapowazia jambo hilo katika siku hii tunayoishi, inayoitwa elimu! Hata huwezi kwenda mimbarani isipokuwa uwe na Shahada ya Udaktari, na kadhalika.

²³¹ Inanikumbusha juu ya kasisi mmoja, wakati mmoja, aliyekuwa anatoka katika jeshi. Akasema—akasema, “Ndugu Branham, ilikuwa ni mara baada ya Vita vya Kwanza vya Dunia.” Kasema, huyo kasisi akasema, “Sajini alipitia pale na kusema, ‘Kasisi, unataka kupanda gari twende pamoja kwenye mstari wa mbele wa vita, huko Argonne,’” kule kutoka La Salle, Lorraine, Ufaransa, unajua. Naye akasema, “Nilitoka

nikaenda kwenye Msitu wa Argonne.” Naye akasema, “Alikuwa akichukua idadi ya vifaru kadhaa vilivyokuwa vimelipuliwa.”

²³² Ndipo akasema, “Ilikuwa ni kwenye asubuhi ya Pasaka.” Kasema, “Ndiyo kwanza nimalize... Nilipita pale pamoja na nesi mmoja, naye alikuwa akiwapa hao vijana waliokuwa wamejeruhiwa, waridi la Marekani, unajua, ua fulani ambalo Mmarekani alikuwa amelizoea. Hao vijana walilinyakua waridi hilo, na kupiga tu makelele na kulia, maana walijua lilitoka nyumbani.” Unaona, lilikuwa limetoka nyumbani.

²³³ Na hivyo ndivyo ninavyofikiri tunavyofanya na Neno, unaona, tunalinyakua, “Ee Mungu!” Linatoka Nyumbani, unaona.

²³⁴ Kasema, “Niliwaona, wakihemkwa. Humu moyoni mwangu...” Akasema, “Nilitoka nikaenda huko nje na kusema... Naye yule—yule kapteni akatoka akaenda huko nje kuchukua idadi ya vifaru vilivyokuwa vimeangamizwa, na vitu kama hivyo.” Kasema, “Roho Mtakatifu akasema, ‘Nenda pale kwenye lile jiwe dogo.’” Naye akaangalia pande zote. Kasema, “Walirusha ile sumu ya mvuke na gesi ya klorini na,” kasema, “vikaunguza majani yote kutoka kwenye miti. Hapakuwapo na kitu kilicho hai kilichosalia, na ilikuwa ni Pasaka!” Akasema, “Ni Pasaka ya namna gani! Ni Pasaka ya namna gani, wakati hakuna hata nyasi ardhini, wala chochote kile!” Naye akasema kitu fulani kilimvutia kwenye jiwe fulani. Akalipindua hilo jiwe, akasema, “Kulikuwa na ua dogo la Pasaka chini yake, lililokuwa limelindwa chini ya hilo jiwe, wakati wote wa hiyo gesi ya sumu.” Ndipo kasema, “Nikawazia, ‘Ee Mungu, nilinde chini ya Mwamba wenye Imara, mpaka sumu hii yote itakapokwisha, na nijalie nichanue katika ile Nchi huko ng’ambo.’”

²³⁵ Tungeweza kusimama hapa kabisa, mkitaka, maana ni—nina mambo mengi sana hapa, nisingeweza kamwe kuyafikia, hata hivyo, mnaona, kuhusu mambo kadhaa. Kwa hiyo labda ninaweza kurudi tena na kuyaelezea kwenu.

²³⁶ Loo, nilimaliza kuhubiri tu hivi majuzi, “*Chujio la Mtu Mwenye Busara*,” ninyi nyote mmeusoma Huo, mnaona, “linaleta ladha ya mtu mtakatifu.” Wazieni, enyi ndugu. Lolote mfanyalo, wazieni! Waefeso 5:26, hapo ndani ilichosema.

²³⁷ Nasi tulikuwa tumezungumza, tumezungumza juu ya neno la *kuchaguliwa tangu zamani*, mnaona, hilo linawakwaza watu wengi sana. Ni Neno la Mungu. Yeye, Yeye analitumia, “kwa kuwa tumechaguliwa tangu zamani kwa Neno la Mungu.” Nalo, kwa kuwa sisi... Unapochaguliwa tangu zamani, mbona, lazima litukie, kwa kuwa hivyo ndivyo ilivyo. Mungu, Mungu alikuchagua kwa sababu alijua utakachofanya tangu mwanzo.

²³⁸ Wala usimwache Ibilisi akunyunyizie elimu na sumu, na upuuzi kama huo, “Inakubidi uwe wa kisasa. Inakupasa uwe *hivi*.” Haiwabidi kuwa chochote kile ila wana na binti za Mungu.

Na kama mmezaliwa kwa Neno, unakuwa hivyo. Angalia manyunyu hayo. Kama ukichukua mbegu, mbegu nzuri na uipige dawa, ita—itaia. Na wakati wanaponyunyizia upuuzi huu wa kimadhehebu juu yako, itaharibu ushawishi wa Neno la kweli. Kama wakikwambia, “Inakupasa kufanya *hivi*. Mbona, hao wasichana wengine wanafanya hivyo. Wanaume wengine wanafanya hivyo.” Usiamini jambo hilo. Litaharibu ushawishi wa Mungu wa Neno Lake juu yako. Unajua jambo hilo.

²³⁹ Fungu letu linasema, “Msiifuatishe,” kunyunyiziwa, “bali mgeuzwe,” mbegu iliyo ndani yako.

²⁴⁰ Watu wa siku hizi wanafanya kana kwamba hata hawaamini kuna Mungu. Je! mlijua jambo hilo? Wanafanya hivyo. Sasa, sitaki kuwaita wao ni wapumbavu, bali wanafanya mambo kama wapumbavu. Maana, Zaburi 14:1 inasema, “Mpumbavu amesema moyoni, Hakuna Mungu.” Hupaswi kumwita mtu ni mpumbavu. Lakini bila shaka wanatenda mambo kana kwamba wao ni wapumbavu, maana hawaninii. . . Wanafanya mambo kana kwamba hakuna Mungu. Neno hili linapuuzwa tu.

²⁴¹ Angalia, hapa hivi majuzi, waliniita chumbani kuangalia. . . Billy Paul, ninaamini, ama baadhi yao, walikuwa wamesema kulikuwa na kipindi cha di—dini kwenye televisheni.

²⁴² Sisi hatuna televisheni. Hakutakuwa na moja nyumbani mwangu, la hashu. Lakini kulikuwa na ninii. . . Ukizitaka, hiyo ni juu yako. Bali Mungu aliniambia nisiwe nayo.

²⁴³ Ndipo wakati tulipohamia kule, nilipangisha kutoka kwa maskini dada huyu mzuri kule, alikuwa na televisheni kwa maana iliwabidi kuwa nayo apate kukodisha nyumba yake. Nami nikawaruhusu kuangalia kipindi fulani cha kidini, kwa hiyo wao—wao waliniita na kusema kipindi cha nyimbo za Injili kilikuwa kinaendelea.

²⁴⁴ Nanyi mnazungumza juu ya kundi la akina Ricky, juu kule wakitenda kama walivyotenda, wakijiita waimbaji wa nyimbo za Injili! Ilikuwa ni kumwaibisha Yesu Kristo, kuona jinsi walivyokuwa wakifanya yasiyofaa, wakijitikisa, na—na mtindo huu wa Kiriike wa kukata nywele na kadhalika, unajua. Ninii tu, ni ninii tu—ilionekana tu—ilionekana kama kwamba ilikuwa ni dhihaka tu!

²⁴⁵ Kaini alikuwa ni mtu wa namna hiyo, wa kidini kwa matendo, bila shaka. Bali alikuwa na mbegu mbaya ndani yake, unaona, na kwa hiyo ilileta uzao wa nyoka. Shetani alikuwa amevuma juu ya uzao huu wa Edeni, na huo ndio uliomzaa Kaini. Aliweka sumu yake juu yake.

²⁴⁶ Yeye, Kaini, alijua mapenzi makamilifu ya Mungu. Alijua mapenzi makamilifu ya Mungu. Kaini aliyajua. Kwa nini? Lakini, alikataa kuyatekeleza, alithibitisha basi kwamba yeye ni uzao wa nyoka. Wakati alipoona mapenzi makamilifu ya Mungu, yeye aliyakataa. Alikuwa amemwona Mungu akiuthibitisha

ujumbe wa Habili. Yeye alijua hayo yalikuwa ni mapenzi ya Mungu. Unaona? Alimwona Mungu akiuthibitisha ujumbe wa Habili. Basi Mungu alimwambia nini? Naye alininii tu, Yeye alisema, “Fanya jambo lilo hilo, abudu kama ndugu yako, na—nawe utafanya vema.” Lakini unaona, yeye aliona mapenzi makamilifu ya Mungu, bali hakuyataka. Unaona, alitaka kuongeza kitu fulani kwake.

²⁴⁷ Nao hawa wanathiolojia wanaona Biblia hii, wanaisoma, bali hawataki kuyatekeleza Hayo. Unaona? Inaonyesha uzao wa nyoka. Wameliona likithibitishwa, na kwa urahisi sana mbele ya watu, bali inaonekana kana kwamba ni vigumu sana kwa watu kujinyenyekeza kwa Neno la Mungu.

²⁴⁸ Hivi ninyi nyote hamwoni, enyi wanawake, wakati mnapowazungumzia wasichana, kuhusu kuwa na nywele ndefu, nao wanasema, “Kwa nini una nywele ndefu?” Unaona? “Kwa nini mnavaa sketi zilizorefuka, ndefu?” Ukianza kuwazungumzia, kwa namna fulani wanakupuuza. Hiyo si ni kweli? Unaona, wao wanajua jambo hilo ni sawa, kama kuna—kama kuna ubibi wowote ndani yao. Unaona? Wanajua jambo hilo ni sawa. Lakini, unaona, hawawezi kujinyenyekeza kwa jambo Hilo. Unaona, hivyo ndivyo ilivyo.

²⁴⁹ Unaona jinsi Kaini alivyofanya? Hakuweza kujidhili kwa Neno la Mungu lililothibitishwa. Asingeweza kufanya jambo hilo.

²⁵⁰ Loo, hata Wapentekoste wanasema, “Utukufu kwa Mungu! Haleluya! Ninakata nywele zangu, na kunena kwa lugha!” A-ha! Hiyo inaonyesha papo hapo kuna kasoro fulani, unaona, hiyo mbegu inazaa kitu fulani tofauti.

²⁵¹ Mbegu haiwezi. Mbegu ya Mungu haiwezi kuzaa mwanamke aliyekata nywele zake. Haiwezi kufanya jambo hilo. Haiwezi kabisa kufanya hivyo, maana Biblia ilisema hivyo. Unaona, haiwezi kufanya hivyo. La, bwana.

Sasa inaonekana ni vigumu sana kujinyenyekeza kwenye Neno la Mungu.

²⁵² Angalia hilo katika Mwanzo 4:6 na 7, tukisoma tu Maandiko fulani hapa. “Fanya kama Habili alivyofanya.” Alisema, “Kama u—ukiona vile ndugu yako...” Kasema, “Endelea na ukafanye vile Habili alivyofanya, fanya namna hiyo hiyo ya ibada aliyofanya, Na—Nami nitakubariki. Usipofanya hivyo, dhambi inakuotea mlangoni.” Sasa, *dhambi* ni “kutokuamini.” “Usipofanya kama vile Habili alivyofanya! Umeona nimemthibitisha, na nimemhesabu kuwa ni mwenye haki. Sasa usipofanya hivyo, basi inaonyesha ya kwamba—ya kwamba dhambi, kutokuamini, kunakuotea mlangoni.” Unaona?

²⁵³ Na siku hizi wanaona yale Mungu anayothibitisha. Wanaona vile Mungu anavyofanya. Wanaona mambo haya

yote yakitendeka. Wanajua habari za mambo haya. Mungu anaonyesha ishara Zake mbinguni juu na chini duniani, na mambo haya yote namna hiyo, nao wanaona yale yanayotukia. Bali hawatafanya jambo hilo. Unaona, Shetani, uzao wa nyoka; werevu, wanatoka katika seminari, wameelimishwa vilivyo, kila neno, kila kitu, wanasimama mimbarani vizuri kabisa, na kila Neno halina budi kuwa sawasawa, sarufi haina budi kuwa sawa, na kila kitu vivyo hivyo. Unaona? Hakika, hawawezi kujinyenyekeza, jamaa kama huyo. Unaona, hawawezi kamwe kufanya jambo hilo. Hawalifanyi. Hawawezi kulifanya kabisa.

²⁵⁴ Sasa, “Vingenevyo, dhambi inakuotea mlangoni; kutokuamini kunakuotea,” ndipo akawa asiyetii makusudi. “Na unapojua kutenda jema, na usilitende, kwako ni dhambi,” kama unajua yaliyo mema wala huyafanyi. Unaona? Ndipo akawa asiyetii makusudi baada ya Neno kuthibitishwa, ndipo akavuka mstari wa utangano, ndipo akafukuzwa kutoka Edeni wakati alipouvuka. Kuna mstari ambapo unaenda umbali fulani, na, kama ukienda mbali zaidi upande huo mwingine, umetoka nje. Unajua jambo hilo, sivyo? Kuna mstari. Kama huamini jambo hilo, hebu soma Waebrania 10:26. Hayo ndiyo Maandiko niliyokuwa nikiyarejea pale, unaona.

*Maana, kama tukifanya dhambi kusudi baada ya . . .
kuupokea ujuzi wa ile kweli, haibaki tena dhabihu kwa
ajili ya dhambi;*

²⁵⁵ Hilo ni Agano Jipya. Hiyo ni kweli? “Kama tukifanya dhambi kusudi baada ya kuupokea Ujuzi ambao mmehubiriwa, umesomwa kwenu, umethibitishwa kwenu; baada ya kuona ujuzi wa ile Kweli, na unaendelea na usiamini, kusudi, hakuna tena thabihu kwa ajili ya dhambi.”

*Bali . . . kuna kuitazamia . . . hukumu kwenye kutisha,
ukali wa moto ulio tayari kuwala wao wapingao.*

²⁵⁶ Je! hiyo ni kweli? Unaweza kuuvuka mstari huo. Kama vile wana wa Israeli walivyofanya katika safari yao, wakija kupitia nyikani, Israeli walifanya vivyo hivyo. Baada ya kuusikia ujumbe wa Musa na kuoona ukithibitishwa; wakamsikiliza nabii wa uongo aliyesema, “Loo, sasa angalieni, enyi watoto, sisi sote ni sawa. Tunapaswa kuoana sisi kwa sisi, na tunapasa kufanya hivi.” Naye Musa alikwishawaambia vinginevyo, na wakaona Mungu akilithibitisha. Kwa sababu, Balaamu alionekana kuwa mtu mwenye kuelezea mambo vizuri zaidi kuliko vile Musa alivyokuwa, unaona. Yeye alikuwa ametoka katika taifa kuu ambako kulikuwa na watu mashuhuri, nao wote walikuwa wamejiratibu pamoja katika utaratibu, ile nchi ya Moabu, majeshi makubwa, na mambo makubwa ambayo watu katika siku hizo wangeyaogopa. Na huyu hapa nabii anakuja, nabii, aliyepakwa mafuta, nabii wa uongo aliyetiwa mafuta, unaona, akashuka akaja kwa aliyetiwa mafuta (angalia jinsi walivyofanana), na akawafundisha watu, na

wengi wao wakamfuata huyo. Kamwe msisahau jambo hilo. Unaona, wakafuata jambo lile ambalo halikuwa ni Neno, Neno lililothibitishwa na kuhakikishwa!

²⁵⁷ Msiruhusu mtu fulani aje aingie hapa na kuwaambia jambo la tofauti. Angalia yale Mungu anayothibitisha na kuhakikisha.

²⁵⁸ Sasa kama watu hao wangaliangalia nyuma, na kusema, “Musa! Mungu alionekana mbinguni. Na mtu huyo alinena na kukatokea, viroboto, nzi, vyura; akaondolea mbali, majipu na magonjwa. Akafungua Bahari ya Shamu, nasi tukaja... Na akatulisha mana kutoka mbinguni. Loo, huyo ndiye nabii wetu!”

²⁵⁹ Bali huyu hapa nabii mwingine akashuka akaja, “Utukufu kwa Mungu! Mimi ni nabii, pia.” Akasema, “Sasa, ninyi nyote, nitawaambia. Sasa, sasa mnaelewa, ninatumia sarufi bora zaidi kuliko Musa. Nami niko *hivi* na *vile*, mnaona,” na kadhalika.

²⁶⁰ Na muda si muda unajua, wakashawishika. Na kila mmoja wao akaangamia mumo humo nyikani. Hakuna hata mmoja wao aliyesalia. Hakuna. Hawatakuwa Mbinguni, hata mmoja wao. Yesu alisema.

²⁶¹ Wao walisema, “Baba zetu walikula mana nyikani!” Unaona, Wapentekoste, ni kweli, unaona, walikuwa kweli wamepitia kwenye matukio yote. Wao, “Baba zetu walikula mana nyikani!”

²⁶² Akasema, “Nao, kila mmoja wao, amekufa.” *Mauti* ni “Kutengwa milele.” Hawataishi tena, hata ingawa walikuwa wamepitia katika matukio haya yote. Tukinena kimfano, walikuwa wamenena kwa lugha, na kucheza katika Roho, na kila kitu.

²⁶³ Lakini wakati ilipofikia kwenye onyesho la kuamua kati ya Neno kati ya manabii wawili, mmoja wao akiwa amesimama na Neno, na huyo mwingine alikuwa nje ya Neno; wote wawili, manabii. Mnaelewa? Semeni, “Amina.” [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Mmoja kwenye Neno, na huyo mwingine nje ya Neno; wote wawili, manabii, wamehibitishwa kuwa manabii. Lakini mmoja alikuwa ana Neno, unaona. Wapakwa mafuta wa uongo katika siku za mwisho, unaona. Mmoja... Manabii, wote wawili, manabii; mmoja yuko kwenye Neno na mmoja (mmoja) aliyethibitishwa kwa Neno, na huyo mwingine hakuwa amethibitishwa kwa Neno. Kaini na Habili, tena. Unaona hao wawili, wa uongo—wa uongo na wa kweli? Vema.

²⁶⁴ Lakini kila mmoja wao aliozea nyikani, na akaangamia. Nafsi zao zimekufa, na zimeangamia. Nao wako kabisa katika wajibu wa kazi, wakienda kanisani na ndiyo mambo yale kabisa ambayo Mungu aliwaagiza kufanya, bali walimkubali mwalimu wa uongo, ambaye hakuwa amethibitishwa kwa Neno, kuthibitishwa kwamba alikuwa sahihi. Hata hivyo, yeye alikuwa Daktari wa Mambo ya Uungu, na chochote kile zaidi unachotaka kuita kuhusu nabii halisi, bali hakuwa amethibitishwa kiroho

kwa Neno na kwa ishara za Mungu. Nao waliangamia nyikani; watu wenye haki, wa heshima, wa kidini, wakafa, wala hawatakuwako Mbinguni.

²⁶⁵ Unaona mahali tunapopaswa kutembea? Mnaelewa? [Kusanyiko linasema, “Naam.”—Mh.] Msiache jambo hilo liponyoke.

²⁶⁶ Ni sawa na vile ilivyokuwa katika nyakati za Neno-mbegu la Nuhu lilivyojenga mageuzi yaliyoelea kutoka duniani mpaka mbinguni. Lilisikika kana kwamba ni wenda wazimu kwa watu, kuwa na kikundi kidogo kama Nuhu alivyokuwa nacho. Naye akawaambia, akasema, “BWANA ASEMA HIVI. Mungu amenena, na mvua inakuja.”

²⁶⁷ Sayansi, na wasomi na wanadini wa siku hizo, walisema, “Mwangalieni maskini yule mzee bingwatapeli. Anazeeka, akili yake inasepetuka.”

²⁶⁸ Unaona, bali alikuwa sahihi, kwa sababu alikuwa ni nabii aliyethibitishwa. Halafu basi, mwishoni mwa wakati, ujumbe wake kweli ulithibitishwa. Angefanya nini? Aligeuza kutoka duniani hadi Utukufuni, kwa safina, ya Neno alilokuwa akihubiri. Liligeuzwa.

²⁶⁹ Manyunyuyu ya kisayansi yaliwaozesha hao wengine kuwaingiza katika hukumu. Waliozea juu ya maji ya hukumu, ya ile gharika.

²⁷⁰ Watu wanajaribu kufanya nini leo, katika wakati huu maarufu wa sayansi wa elimu, kanisa la Edeni, limerejeshwa tena kwenye Edeni yake, kwenye hali ya kisayansi, badala ya Neno? Je! wanalitukuza Neno la Mungu? Je! watu wanajaribu kulitukuza Neno la Mungu, ama je! wanajaribu kujitukuza wenyewe? Lipi ni lipi? sijui?

²⁷¹ Kanisa ni mbegu iliyoharibika: maarifa, mpango, umesababisha jamii yote tena, kwa mambo ya kisayansi, kuwa wajinga kisayansi wa Neno la Mungu. Wajinga kisayansi wa Neno la Mungu! Hilo ni fungu kubwa ambalo ni la kusikitisha, sivyo? Lakini, ndivyo walivyo.

Ati unasema, “Haiwezekani”?

²⁷² Ilikuwa wakati Yesu alipokuja. Siku aliyokuja Yesu, hao—hao watu walilijua hilo Neno la Mungu, kwa Andiko tu. Sivyo? Hakika. Bali hawakujua kwamba Yeye alikuwa ni Nani, walipomwona Mungu juu ya mbawa za hua, akitenda na kufanya vile vile kabisa Yeye alivyosema angefanya. Naye alifanya vile hasa Neno lilivyosema. “Nisipozitenda kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi.” Bali alifanya tu kama vile Neno lilivyosema angefanya. Nao walikuwa ni wanasayansi katika siku hizo, bali walikuwa mbumbumbu kisayansi, kufanya dhambi makusudi.

²⁷³ Ukwere ulikuwa umewapofusha. Wanahitaji Neno la Mungu kuuonyesha, kuuonyesha uchi wake. Katika Ufunuo 3, alisema,

“Nakupa shauri ununue Kwangu dawa ya macho ya kujipaka, ili ufunguliwe macho upate kuona uchi wako.”

²⁷⁴ Dawa hiyo ya macho ni Neno la Mungu, kuponywa kwa macho kunakokutoa kwenye mambo ya maumbile ya kawaida ya dunia, na kukugeuza, kwa nguvu za Mungu, kukuingiza katika Uwepo Wake. Ndipo unaona! Unasema, “Wakati mmoja nilikuwa nimepotea, sasa nimepatikana. Nilikuwa kipofu, bali sasa ninaona.” Unaona, ingekuwa ni tofauti.

²⁷⁵ Hivyo ndivyo wito wa kanisa ulivyo leo, ni, “Ninakupa shauri uje ununue Kwangu dawa ya macho ya kujipaka, upate kupakwa kwa dawa Yangu ya macho, na ndipo utaona.”

²⁷⁶ Hebu acha Roho Mtakatifu ashuke juu ya mtu yeyote ambaye kweli ana kitu fulani hapa ndani! Uponyaji huja kutoka ndani. Hebu huo uponyaji na utoke kutoka katika Roho aliye ndani yako. Kama ni Roho halisi akitia mafuta Mbegu halisi, haiwezi kufanya kitu bali kuzaa mwana ama binti wa Mungu. Lakini Roho halisi anaweza kuja juu ya mbegu ya gu—gugu, mvua inaweza kulinyeshea gugu, na italifanya liishi vile vile hasa kama inavyoineshea ngano na kuifanya iishi. “Bali kwa matunda yao mnawatambua.” Unaona? Sisi ni mti wa matunda, wa Mungu, unaozaa Neno Lake.

²⁷⁷ Yesu alisema, “Mtu na ajikane mwenyewe, na anifuata Mimi. Hebu na akane elimu yake, akane maarifa yake, akane digrii zake; autwae msalaba wake na kunifuata Mimi.”

²⁷⁸ Watu wamepoteza mawazo yao ya kawaida ya mwenendo mwema. Ninafuatilia Maandiko machache hapa chini, kwa ajili ya ninii tu... Nilikuwa nijichukulie kama dakika tano juu yake, kumi, unaona. Watu wamepoteza mienendo yao ya adabu ya kawaida miongoni mwa wao kwa wao. Ha—hawako kama walivyokuwa. Mwanaume wa rika, langu na la ndugu hapa, wanajua, na pia wanawake. Watu hawajiheshimu kama walivyokuwa huko nyuma. Wamepoteza akili za utu wao wa kawaida. A—a—athari—athari ya akili ambayo imewapata watu wa siku hizi za sasa za sayansi tunazoishi, imewasababisha watu kupoteza upambanuzi wao wa kiasilia wa mawazo. Hawawezi kumheshimu mtu, mwanamke, kama dada na ndugu. Ni kitu fulani kichafu. Mara wanaponinii. . .

²⁷⁹ Na wanawake wanafurahia kuvaa kifisadi sana, ili watoke nje miongoni mwa watu. Nao wanasema, “Mimi ni mwanamke mwadilifu.” Vema, kwa nini anajianika huko nje namna hiyo? Yeye amepofushwa. Vema, kama—kama nanii yako... Kama mmoja wa hawa dada hapa, wa—wa umri mdogo, kama mama yako ama mama yangu wangelitoka nje mtaani, jinsi wafanyavyo mmoja wa wanawake hawa, wangelimweka katika asasi ya wenda wazimu; hata hakuwa na fahamu za kutosha kujua kuvaa nguo zake. Vema, kama ilikuwa ni wazimu wakati huo, ni wazimu sasa. Angali ni mwanamke wa aina ile ile. Unaona?

Lakini wamepoteza adabu zao zote, akili zao zote timamu. Wamezipoteza. Na kwa ujuzi wa kisasa, pamoja na utamaduni na elimu, “Ni hali bora zaidi kiafya, kuwa hivyo.” Ni dhambi na ni mauti! Angalia. Wao ni ninii, loo, si kama walivyokuwa huko nyuma. Wakati ninii . . .

²⁸⁰ Na angalia katika maisha ya kanisa. Ilikuwa ni kawaida kwamba, katika maisha ya kawaida ya kanisa, huko nyuma, wakati nabii alipokuwa na jambo fulani la kusema, BWANA ASEMA HIVI, watu walitetemeka. Walishikilia jambo Hilo. Walitetemeka. Lakini sasa siku hizi, “Yule jamaa mimi simpendi. Mwondoeni kwa kura.” A-ha! Mnaona? A-ha. Unaona, hawana akili timamu tena. Watu hawatetemeshwi tena na Roho wa Mungu.

²⁸¹ Neno la Mungu ni Roho Wake, nalo Neno Lake humjia nabii Wake. Nalo Neno linapaswa kuwageuza ninyi kutoka vile mambo ya ulimwengu yalivyo, kuwa sura ya wana na mabinti za Mungu. Na Neno linaweza tu kuwajilia kupitia kwa hawa manabii, walipokuwa wakinena. Na ilibidi yalinganishwe na Neno, na kuonyesha ya kwamba yalikuwa ni Neno. Ndipo kama ukilikubali hilo Neno, litakugeuza; kutoka mwana wa Mungu, ama binti . . . ama, kutoka mwana wa dunia, binti ya dunia, kuwa mwana na binti ya Mungu.

²⁸² Hebu jiangalie hapa ndani. Ni wangapi wamekwisha kupata ujuzi huo? Kila mmoja wetu. Tumekuwa na ujuzi huo. Kwa sababu, lilinenwa, liliaminiwa, nalo Neno likatokea na kuanguka kuingia kwenye tuta la moyo, na hapo likakua moja kwa moja kutoka kwake. Unaona?

²⁸³ Kugeuzwa wewe mwenyewe, Roho Wake Mtakatifu analigeuza lile Neno mbegu likawa katika sura Yake. Kama vile mpea unavyozaa pea, mtofaa tofaa, vitu kama hivyo; Neno Lake litazaa wana na binti za Mungu. Hivyo ndivyo linavyopaswa kufanya.

²⁸⁴ Siku moja wakati dunia ilipokaa katika giza na machafuko tena, Roho ya Mungu alitulia juu, katika mbegu iliyochaguliwa tangu zamani. Mbegu iliyokusudiwa, iliyokusudiwa, iligeuzwa. Ilichukua Isaya 9:6.

²⁸⁵ Sasa, yule nabii akiwa amesimama pale, alikuwa ni m—mtu wa namna gani aliyeyatikisa mataifa, hao watu. Watu wa kidini wa siku yake walimwamini; si wote, hawakumwamini kabisa. Lakini, nabii huyu, walikuwa wamemwona mtu huyo akinena mambo na ilikuwa ni kweli kabisa. Aliyosema yalikuwa makamilifu, na yalitimia. Na, hapa, mtu huyu hana budi kusimama mbele za watu wake, na kusema, “Bikira atachukua mimba,” loo, haliwaziki. Lakini, unaona, Mungu hakulinena, Yeye Mwenyewe, Yeye hulinena kupitia kwa manabii Wake. Sasa, hakukuwa na kitu kilichoandikwa katika Biblia kuhusu jambo hilo, bali nabii huyu alisimama, akasema, “Bikira

ata-..." Katika Isaya 9:6, "Kwa ajili yetu Mtoto amezaliwa, tumepewa mtoto Mwanamume; ataitwa Jina Lake 'Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu Mwenye Nguvu, Baba wa Milele.'" Sasa kama "bikira atachukua mimba," Neno hilo lilinenwa, ambalo lilikuwa ni mbegu, tuta linapaswa kuwapo lipate kuipokea hiyo mbegu, siku moja. Yeye alitafuta katika nchi zote, halikuwapo. Alipitia nchini, halikuwapo.

²⁸⁶ Na karibu kabisa miaka mia nane baadaye, hiyo mbegu iliyokusudiwa ilipata tuta, nayo ikaanza kukua.

²⁸⁷ Ni kama tu vile Mungu alivyofanya hapo mwanzo, "Na iwe nuru," na labda miaka mia nane baadaye nuru ilikuja. "Na kuwe na mti," ukatokea namna hiyo tena, kila kitu alichosema.

²⁸⁸ Hii hapa mbegu iliyokusudiwa ikimzaa *Imanueli*, "Mungu pamoja nasi." "Mataifa watamtafuta," na Huyo Ndiye tunayemtafuta siku hizi, Yesu. Unaona, mbegu iliyokusudiwa!

²⁸⁹ Shetani alijaribu kuinyunyizia, kama alivyomfanyia Hawa. Alijaribu kuinyunyiza, bali alishindwa. Akiwa na kiwinga chake *hapa*, Yeye alikuwa ni mbegu iliyokusudiwa. Wasingeweza kumchukua, kumfanya Farisayo au Sadukayo. Hawakuweza kumfanya awe mfuasi wa madhehebu yoyote. Alikuwa ni Neno la Mungu lililokusudiwa, lililonenwa. Shetani hakuweza kumtupia kutokuamini kwake juu Yake. Alikuwa na kiwinga.

Mungu, tunyunyizie kiwinga, ndilo ombi langu. Hiyo ni kweli.

²⁹⁰ Ndipo Roho akamgusa na kumpeleka Kalvari, msalabani, apate kuleta Nuru katika siku hii, na Nuru kwa mbegu zote zilizokusudiwa kwa Kanisa la siku hii, akiwageuza wana na binti za Mungu wakae Uweponi Mwake.

²⁹¹ Usikwazwe na neno "kukusudiwa." Nimepitia hayo, unaona. Ninataka kuwaonyesha, Waefeso 1:5.

²⁹² Unaona, kama tu ulivyokuwa, angalia, kama tu vile ulivyokuwa ndani ya baba yako; kama nilivyosema hivi majuzi usiku, ni kama tu vile ulivyokuwa ndani ya baba yako hapo mwanzo. Kama usingekuwa, usingekuwa hapa. Lakini, unaona, ilibidi iingie katika tuta la uzazi, kusudi upate kuzaliwa. Na sasa wewe ni mwanawe, wewe ni binti yake. Unaona, ni mbegu. Halafu basi kama wewe ulipata...

²⁹³ Kama wewe ni Mkristo sasa, mbegu halisi iliyochaguliwa tangu zamani, ulikuwa ndani ya Mungu kabla hapajakuwapo na... Daima ulikuwa ndani ya Mungu. Mbegu yako ya uhai, ambayo ni sifa ya Mungu, ambayo ilikuwa ni wazo Lake.

²⁹⁴ Tuseme, kwa mfano, bibi huyu mrembo anayeketi *hapa*, unaona. Mungu alisema, "Katika siku hiyo kutakuwako na msichana fulani, jina lake litakuwa ni *Fulani*. Atakuwa *hivi*, *hivyo*, na *hivi*," na hata alijua hata saa ii hii, "angeketi na kusikiliza Ujumbe, amevaa nguo nyekundu." Unaona, hilo

lilikuwa ni wazo Lake. Hata mume wako awe ni nani, na hata awe ni nani; Naye angeleta jambo hili pamoja, na ungeketi hapa katika—katika huu—katika mji huu siku hii ya leo. Kusingekuwa na njia kwako kukosa hilo, unaona, kwa maana unakua. Na alimradi tu wewe ni mbegu ndani, inayokua, inakubidi kutoa sawasawa na kile hiyo mbegu iliyonenwa ingefanya. Hiyo ni kweli kabisa. Ni Neno Lake; Yeye hutimiza Neno Lake, Analilinda.

²⁹⁵ Ulikuwa katika baba yako, kama mbegu, nawe ukatokea kama binti; wewe, wewe, kila mmoja wenu, ndugu na dada, ndivyo mlivyokuja. Kama hukuwa ndani ya baba yako, basi usingekuwa hapa.

²⁹⁶ Na kama hukuwa ndani ya Mungu... Kama unaamini ujumbe wa Biblia, na Ujumbe huu wa siku hii, thibitisho Lake; sababu ya wewe kuketi hapa, ni kwa sababu ulichaguliwa tangu zamani kuketi hapa. La sivyo, usingekuwa hapa; ungekuwa huko mtaani, labda umelewa, baadhi yenu; na wengine wenu hapa nje na mnazurura kila mahali pamoja na mke wa mtu mwingine; na ninyi wanawake huko nje, mliiolewa, na mnatembea huku na huko na waume wa wanawake wengine, ama kitu kama hicho. Unaona, bali ulikusudiwa kuwa hapa. Unaona, huwezi kujizuia. Una Baba, Yeye ni Mungu, na wewe ulikuwa ni mbegu.

²⁹⁷ Na wakati Yeye alipofikia mahali, amekuweka mahali sasa ambapo... Ulikuwa ndani Yake wakati huo, kama wazo, sasa wewe ni mtu ambaye anaweza kushiriki pamoja Naye. Unaona? Kama vile mlivyokuwa katika ninii, mlivyokuwa katika baba zenu, hapo mwanzo, bali sasa ninyi ni wana na mabinti, kusudi mpate kushirikiana na mzazi wenu. Sasa sisi ni wana na binti za Mungu, ambao tunaweza kushirikiana na Baba yetu, Mungu. Unaona, ni zuri sana! Hivi hamlipendi jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Naam!"—Mh.] Ndipo mkawa kama Yeye. Na kama sisi tulikuwa ni wana, basi ninyi ni sifa, na mlikuwa katika umbo Lake hapo mwanzo.

²⁹⁸ Basi, kumbuka, kama ulikuwa ndani Yake hapo mwanzo; na wakati Yesu, ambaye ni Mungu, Neno lililofanyika mwili na kukaa kwetu; basi ulikuwa ndani Yake na ukastahimili matusi aliyostahimili. Ulikwenda Kalvari pamoja Naye, ukiwa ndani Yake. Ulikufa, katika Yeye. Ulifufuka, katika Yeye. Na sasa mmeketi pamoja katika ulimwengu wa Roho, katika Yeye. Unaona?

²⁹⁹ Kama mimi ni Mmarekani, ninawakilisha aibu yake yote, ninawakilisha utukufu wake wote. Chochote ilichowahi kuwa, ndicho nilicho. Mimi ni mwananchi wa Marekani. Nilikuwa... Nilishuka huko Plymouth Rock. Naam, bwana. Naam, nilishukia huko Plymouth Rock. Nilitia sahihi ile... Nilikuwa kwenye ule ukumbi asubuhi hiyo hapo walipotia sahihi Azimio la Uhuru. Nililitia sahihi pamoja nao. Mimi ni sehemu ya mpango wake. Nilitia sahihi Azimio hilo ama Uhuru. Hiyo

ni kweli. Nilikuwa pamoja na Washington, huko Valley Forge, wakati alipovuka ule mto. Nilikuwapo asubuhi hiyo. Niliomba pamoja naye. Nilikuwapo. Ulikuwapo, kama Mmarekani. Kama wewe ni Mwamerika, ulikuwapo. Kwa kuwa, cho chote Amerika ilicho, ndivyo ulivyo wewe. Nilipandisha bendera—bendera huko Guam. Niliwasaidia kufanya jambo hilo. Niliteka kila ngome. Nilichukua aibu yake, kama mwanamapinduzi. Cho chote ilichokuwa, ndicho nilicho mimi.

³⁰⁰ Na cho chote Kristo alichokuwa, ndicho nilicho mimi. Kile alichu Yeye, ndicho nilicho. Ee Mungu! Kama anahesabiwa kuwa ni mshupavu wa dini, ndivyo ninavyopaswa kuhesabiwa. Kama alikuwa Be—Beelzebuli, kwa kazi Zake za Roho Wake, ndivyo mimi pia nilivyo. Chochote alichokuwa, ndicho nilicho mimi. Chochote alichokuwa, ndicho ulicho wewe.

³⁰¹ Hatuna budi kuwa wenye kubuni kutokupatikana na mauti kwake, uhuru wake ama sifa zake, utukufu wake ama aibu yake.

³⁰² Hatuna budi kuwa hivyo. Hatuna budi kuwa Kanisa, Bibi-arusi wa Yesu Kristo. Niliishi pamoja Naye duniani, wakati alipoishi. Nilikufa pamoja Naye wakati alipokufa. Nilifufuka pamoja naye alipofufuka. Nimekusanyika na nimeketi pamoja Naye katika ulimwengu wa Roho, kwa kuwa mimi ni sehemu Yake. Popote alipo, hapo nipo. “Mahali alipo mtumishi Wangu, nitakuwa hapo pia.”

³⁰³ Sasa Yeye anaweza kufanya ushirika na sisi na katika sisi, na kuweka Neno Lake kwetu. Ambapo, sisi ni sehemu ya Neno Lake. Sisi . . . Na kama Yeye ni Neno, na sisi ni sehemu Yake, basi sisi ni sehemu ya Neno.

³⁰⁴ Na ninawezaje kukana kwamba nina mkono? Haidhuru ni jinsi gani juha fulani angeninii, samahani, sayansi fulani ingesema, ya kwamba—ya kwamba sina mkono; nina mkono! Ninajua nina mkono. Ninautumia.

³⁰⁵ Na ninajua nina Mungu. Nina Mwokozi. Ninamhisi nafisini mwangu. Mimi, mimi ni sehemu Yake. Hivyo ndivyo Neno hili linavyosema, hivyo ndivyo nilivyo. Na kama nikikana sehemu moja ya *Hili*, hiyo ingekuwa ni kama kukana nina mkono, sikio, jicho. Nisingeweza kufanya hivyo na kubakia mwanadamu, nikiwa na akili zangu timamu; wala siwezi kukana Neno lolote la Mungu na nibaki nikiwa na ninii, Roho halisi ya Mungu. Inanibidi kuchukua yale madhehebu yanayosema ama yale Mungu aliyosema kuhusu jambo Hilo. Unaona? Huwezi kufanya hivyo.

³⁰⁶ Sasa, “kugeuzwa.” Yeye anaweza kutugeuza kupitia Neno Lake, hivi kwamba tupate kupumzika, kwa maana sisi ni sehemu Yake.

³⁰⁷ Na sasa kuna mambo mengi, katika kuzungumza juu ya kuzaliwa kwangu kwa kawaida, kuna mambo mengi katika kuzaliwa kwangu kwa kawaida ambayo nisingeweza kujivunia.

Nitawaambia, sina kitu cha kujivunia. Mama yangu alikuwa ni mwenye dhambi, kwanza; baba yangu alikuwa ni mwenye dhambi. Nao walitoka katika kundi la wauaji na wapiganaji wa bunduki, na karibu wote walikufa wakiwa wamevaa buti zao; walevi na watengenezaji wa pombe haramu, na chochote kile, wanatokea Kentucky. Mama yangu, nusu Mhindi. Na mimi si—sina kitu cha kujivunia. Siwezi kujivunia ukoo wa familia yangu.

³⁰⁸ Lakini, utukufu kwa Mungu, kuna jambo moja ninaloweza kujivunia, Kuzaliwa kwangu Mara ya Pili, ambako kunatoka kwa Yesu Kristo. Ninaweza kujivunia Mzazi huyo tuliye naye, kwa kuwa Yeye ni Baba yangu. Yeye ni Mwokozi wangu. Yeye ni Mkombozi wangu. Ninaweza kujivunia kila kitu ambacho—ambacho amenifanyia, kwa maana sasa nimekuwa mwanawe. Mimi si mwana wa Charles Branham tena, mimi ni mwana wa Yesu Kristo. Hiyo ni kweli. Ninaweza kujivunia Kuzaliwa kwangu sasa. Siwezi kujivunia kuzaliwa kwangu kwa kwanza, hakuna kitu, ninaonea aibu jambo hilo. Bali sionei haya Kuzaliwa kwangu Mara ya Pili. La, la. Sionei haya Kuzaliwa kwangu Mara ya Pili. Yeye alifanyaje jambo hilo? “Kwa kuosha kwa maji kwa Neno.” Hiyo ni kweli.

³⁰⁹ Waaminio waliokusudiwa hasa wanadumu na Neno, wala hawatalipotoshwa. Haliwezi kupotoshwa. Loo, enyi wana na binti za Mungu, mbona tusiwe na ushirika huu mkuu tunaopaswa kuwa nao, pamoja na wana wote na binti za Mungu? Tunapaswa kuwa nao. Bali watu hawatafanya jambo hilo kwamwe, ni hivyo tu, kwa kuwa wao si wana na binti wa kweli wa Mungu tangu . . .

³¹⁰ Unaona, kama nilivyosema hivi majuzi usiku, nilikuwa nikienda kuninii. . . Nilikuwa nimeandika hapa chini, bali sina wakati wa kulifikia. Nitaliacha, sasa ninaondoka.

³¹¹ Hicho kitu kidogo cha ndani ya ndani, hapo ndipo unapoanzia, ambayo ni *nafsi* yako; ndipo toka hapo, unakuwa *roho*; na ndipo unakuwa *kiumbe* hai. Sasa, *kiumbe* hai kina hisi tano, za kuwasiliana; ya *pili* ina hisi tano. Huo ni mwili wa nje: kuona, kuonja, kugusa, kunusa, na kusikia. Mwili wa ndani una upendo na dhamiri, na kadhalika, hisi tano. Lakini kule ndani ya ndani, ule mnara wa kuongoza, ni aidha Mungu au Shetani.

³¹² Nawe unaweza kuiga chochote cha vitu hivi unavyoweza kuwasiliana navyo, kama—kama nani—kama vile Mkristo; ama ungeweza kutoa pepo, kama Mkristo. Lakini mnara wa ndani wa kuongoza, lile chimbuko, asili yake, si ya Mungu, kamwe haitarudi kwa Mungu. Mnaelewa na jambo hilo? Je! hivi Yuda hakutoa pepo? Kayafa hakuninii, yule aliyemhukumu Yeye na kumwua, hata kutabiri? Bali hakuweza kutii Neno. Unaona? Hiyo ni kweli.

³¹³ Kugeuzwa kutoka kwenye kanisa na ulimwengu, kuwa wana na binti za Mungu! Angalia jambo hili, katika kufunga sasa.

³¹⁴ Na sasa jinsi ambavyo wana wa Mungu wanaotangatanga, wanaotangatanga huko nje duniani, baadhi yao madhehebu *haya*, kutoka madhehebu hadi madhehebu, kama nyota zinazohamama, hawatulii. Kama jani kwenye maji katika msimu wa kupukutika kwa majani. Tulikuwa tukiona jambo hilo, Leo, kule Mashariki mbali. Majani yangepukutika na kuanguka juu yake, na kila upepo mdogo ungelipeperusha toka upande *huu* kwenda upande *ule*.

³¹⁵ Lakini Mungu anatutaka tuwe thabiti. “Nimetia nanga katika Yesu, nitastahimili dhoruba za maisha. Nimetia nanga katika Yesu, sitaogopa upepo wala wimbi,” unaona, chochote kile. Wengi mnakumbuka ile kengele ya Inch Cape, mlipokuwa shuleni, mvulana na msichana shuleni.

³¹⁶ Mwili wa Ibrahimu na wa Sara ulibadilishwa, upate kutimiza masharti ya Neno lililoahidiwa. Unaona, walikuwa ni wazee. Ibrahimu alikuwa amepokea ahadi, na Sara, wakati Ibrahimu alipokuwa na umri wa miaka sabini na mitano, mkewe alikuwa na umri wa miaka sitini na mitano, amepita wakati wa hedhi; aliishi naye tangu alipokuwa msichana mdogo, alikuwa ni dada yake wa kambo. Na, ili kutimiza ahadi hiyo, miili yao wote wawili iligeuzwa, kutoka kuwa mwanamume mzee na mwanamke mzee, wakawa kijana mwanamume na kijana mwanamke, wapate kutimiza ahadi ya siku hiyo.

³¹⁷ Utukufu kwa Mungu! Hilo linanifanya nijisikie vizuri sana. Unaona? Sijali nilikuwa nini, sijali jinsi nilivyokuja hapa, tunaweza kugeuzwa tupate kutimiza ahadi ya siku hii. Wakati, tunapoweza kukaa pamoja katika umoja na utamu wa Roho Mtakatifu, na kuishi kama ndugu na dada.

³¹⁸ Henoko, mwili wake wote uligeuzwa, apate kutimiza mfano, katika Mungu, naye alitwaliwa Mbinguni bila hata ya kuona mauti, Henoko aligeuzwa. Eliya alifanya jambo lile lile.

³¹⁹ Mwili wa Yesu uligeuzwa kutoka umbile baridi lililokufa, lililopondwapondwa, uliopigwa mpaka majeraha Yake na mbavu Za—Zake zikatokeza mgongoni. Na—na moyo Wake ukatobolewa, kwa mkuki labda ulio mpana namna *hii*, akachomwa kabisa Moyoni Mwake, na Damu na maji yakatoka. Hata unyevu kutoka mwilini Mwake, uliondoka, na Damu ikachuruzika kupitia kwenye mkuki huo, na kudondokea kwenye miguu yake, na ikachuruzikia ardhini. Naye alikuwa amekufa kabisa mpaka mwezi na nyota zikasema alikuwa amekufa, dunia ikasema amekufa; na ikashikwa na wasiwasi mkuu wa neva, ma—mawe yakatetemeka yakatoka ardhini, na kila kitu. Kila kitu kilisema Yeye alikuwa amekufa; hata Mungu aliuficha uso Wake. Alikuwa amekufa. Lakini mwili Wake ulikuwa umegeuzwa. Kwa nini? Kwa sababu Mungu alisema, “Sitaiacha nafsi Yake katika kuzimu, wala sitamwacha Mtakatifu Wangu aone uharibifu.” Hakuna njia ya kufanya jambo hilo.

³²⁰ Panapo siku fulani za usoni, huenda miili yetu ikanyoshwa kwenye jeneza. Huenda tukaja. . . Huenda ukaja na kuniangalia nimelala katika jeneza. Huenda nikaja nikakuangalia, huenda ikanibidi kusema maneno ya mwisho juu yako, ama kitu kama hicho. Bali kamwe hutatuweka kaburini. Huenda watu wakaweka mawe juu yako. Huenda wakakuzika baharini. Huenda wakafanya lolote watakalo, bali nguvu za kugeuza za Mungu. . .

³²¹ Katika Wathesalonike II, ilisema, “Sitaki msijue, ndugu, habari zao waliolala mauti. Kwa kuwa twawaambia haya, pia, kwa amri za Bwana, ya kwamba tarumbeta ya Mungu italia, nao waliolala katika Kristo watafufuka kwanza; sisi tulio hai na tuliosalia,” kama vile wimbo ulivyosema asubuhi ya leo, “tutanyakuliwa pamoja nao, ili tumlaki Bwana hewani.”

³²² Nguvu za kugeuza za Mungu, ambazo zimetutoa kutoka katika machafuko ya sayansi na elimu, na mambo ya dunia, na ujuzi wa siku hii ya kisasa, zimetugeuza sasa tukawa wana na binti za Mungu. Na hata mauti yenyewe hayawezi kamwe kutushikilia kaburini. “Tutabadilishwa, kwa dakika moja, kufumba na kufumbua.”

“Loo, unataka kusema?”

³²³ Ninataka kusema ya kwamba hiyo ni Kweli! Yesu, huyo Neno alisimama duniani, ambaye alikuwa ni Neno, Yule aliyefufuliwa, na akamfufua Lazaro. Yeye alisema, “Mimi ni Ufufuo na Uzima; yeye aniaminiye Mimi, asijakufa, hata hivyo ataishi. Na yeye aishiye na kuniadini Mimi hatakufa kamwe.” Hakuna njia ya kulizua Neno la Mungu lililo hai! Halina budi kufufuka tena.

³²⁴ Na kutoka katika mchafuko huu wa Edeni hii ya kisasa ya kisayansi ambamo tunaishi, ya utamaduni na—na sayansi na elimu, upuuzi huu wote wa kisasa, tutafufuka! “Vazi hili la mwili tutalidondosha, na tutafufuka na kunyakua thawabu ya milele,” siku moja. Tutapitia hewani, na hayo yote yatakwishia. Kwa maana Neno la Mungu ambalo limetuleta kutoka katika mawazo ya kisasa ya nia zetu, likigeuza nia yetu katika kufanya upya mioyo yetu kumwelekea Mungu, na roho zetu; Roho yuyo huyo aliyesema hayo, ametugeuza umbali huu, na pia atatupeleka Mbele za Uwepo Wake, Utukufuni Mwake, tukiwa na mwili wa utukufu.

³²⁵ “Watajenga nyumba, watakaa ndani yake. Watapanda mizabibu.” Katika utafiti wetu wote wa kisayansi; tunapanda shamba, wana wetu wanakuja na kula matunda yake, na wanawe wanakuja na kuchukua kutoka kwake. Nao wanapanda, na mwingine anakula; nao wanajenga, na mwingine anakaa ndani yake. “Bali siku za watumishi wangu zitakuwa nyingi, watakuwa kule pamoja na watoto wao. Watajenga, na mwingine hatakaa ndani yake. Watapanda, wala hakuna mwingine atakula.” Ni nini? Mungu yeye yule, nabii yeye yule ambaye

Neno la Mungu lilisema “bikira atachukua mimba,” alituahidi jambo hili!

³²⁶ Tunalipataje? Tuko hapo sasa kwa uwezo uliositirika, unaona, kwa kuwa Mungu alisema hivyo. Haina budi kuwa. Wakati alipomfufua Lazaro pale, alisema, “Msistaajabie maneno haya, kwa maana saa yaja, ambayo watu wote waliomo makaburini watasikia Sauti ya Mwana wa Adamu, nao watatoka; wengine kwa aibu, na wengine kwa Uzima.”

³²⁷ Ni kitu gani? Kugeuzwa, kugeuzwa na Neno la Mungu, likitufanya wana na binti za Mungu, na pia litatupa Uzima katika ulimwengu ujao. Loo, jamani! Ningesema nini zaidi? Msisikilize mambo mengine.

Usitamani utajiri usio na thamani wa ulimwengu huu,

Ambao huoza haraka sana,

Jenga matumaini yako juu ya mambo ya Milele, Hayatapita kamwe.

Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika! (Hebu tuuimbe!)

Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika! (*Huu hapa!*)

Jenga matumaini yako juu ya mambo ya Milele, Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!

Wakati safari yetu itakapokwisha,

Kama tumekuwa waaminifu kwa Mungu,

Makazi yetu ya Utukufuni maangavu na mazuri,

Nafsi zetu zenye furaha tele zitayaona.

Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika! (Ugeuzwe!)

Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!

Jenga matumaini yako juu ya mambo ya Milele,

Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!

³²⁸ Usiangalie sayansi, yale inayoweza kuthibitisha, kama iko kinyume na Neno. Unaona? Usiangalie kanisa, vile linavyosema, kama liko kinyume na Neno.

Kwa kuwa tunaushikilia mkono wa Mungu usiobadilika!

³²⁹ Nyakati hubadilika, sayansi hubadilika. Ushikilie mkono huo usiobadilika!

Jenga matumaini yako juu ya mambo ya Milele,

Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika.

³³⁰ Baba Mungu, Uweponi Mwako, tunapokusanyika hapa asubuhi ya leo ndani hapa, tukichukua Ujumbe wa kuchosha, mrefu, uliovutwa, na, Ee Bwana, ninaomba ya kwamba utaziweka hizo Mbegu huko nje katika mioyo ya watu hawa.

Kumbuka, Bwana, tunaomba, ya kwamba sisi ni wanyonge, na miili yetu ni minyonge, nasi. . . mara nyingine hatujui tugeuke upande gani. Mungu mpendwa, tugeuze Wewe na utuongoze kwa Roho wako mkuu, Bwana. Tusaidie. Kamwe usituache peke yetu, Baba. Ulihidi hutatuacha. “Sitawaacha wala kuwapungukia. Nitakuwa pamoja nanyi.”

³³¹ Na, Baba Mungu, tunaomba ya kwamba Wewe utamwongoza Ndugu yetu Leo, na Gene. Wafanye, Bwana, aina ya viongozi ambao ungependa wawe juu ya watu hawa hapa; si kutumia mawazo yao wenyewe, bali jalia Roho Mtakatifu mkuu awaongoze katika yale wafanyayo.

³³² Wabariki wanaume hawa na wanawake, watoto hawa wadogo, wanaoonekana, kwangu, Bwana. Nami na—na—naomba ya kwamba Wewe utawadumisha katika maisha marefu. Jalia, kama ikiwezekana, Bwana, jalia tuishi tupate kuona Kuja Kwake. Tunaamini tutaona kuja Kwake, kwa maana tunaona kila kitu kiko karibu sana sasa. Kuko karibu sana! Tujalie, Baba. Tunawakabidhi Kwako, pamoja na sisi wenyewe, sasa, kukutumikia, katika Jina la Yesu. Amina.

Ninasikitika niliwaweka sana hivyo muda mrefu. Ndugu Leo.



NGUVU ZA KUGEUZA SWA65-1031M

(Power Of Transformation)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulitolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili asubuhi, tarehe 31 Oktoba, 1965, katika Bustani ya Misonobari ya Kuegeshea Matrela, huko Prescott Arizona, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2010 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org